
JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA



# KIUNZI CHA UTHIBITI UBORA WA SHULE **KILICHOBORESHWA**

Juni, 2024




## MUHTASARI

**SEHEMU YA KWANZA:**
UTANGULIZI
*Ukurasa 1*

**SEHEMU YA PILI:**
KANUNI NA TARATIBU ZA UTHIBITI UBORA WA SHULE
*Ukurasa 6*

**SEHEMU YA TATU**
UPIMAJI, TATHMINI YA UBORA WA SHULE NA UTOAJI TAARIFA
*Ukurasa 11*

**SEHEMEU YA NNE:**
MFUMO WA UENDESHAJI WA UTHIBITI UBORA WA SHULE
*Ukurasa 17*

**SEHEMU YA TANO:**
UFUATILIAJI, TATHMINI NA UJIFUNZAJI KATIKA UTHIBITI UBORA WA SHULE
*Ukurasa 26*

**SEHEMU YA SITA:**
UTEKELEZAJI WA KIUNZI CHA UTHIBITI UBORA WA SHULE
*Ukurasa 33*

## YALIYOMO

**UTANGULIZI**---------------------------------------------------ii
**SHUKRANI**----------------------------------------------------iv
**UFAFANUZI DHANA MUHIMU** --------------------------v
**VIFUPISHO** ----------------------------------------------- vii

1

**SEHEMU YA KWANZA: UTANGULIZI**
1.1 Usuli -------------------------------------- 1
1.2 Dira na Dhima ya Elimu ------------------ 2
1.3 Urazini ------------------------------------- 3
1.4 Lengo -------------------------------------- 4
1.5 Mawanda ---------------------------------- 4

6

**SEHEMU YA PILI:KANUNI NA TARATIBU ZA UTHIBITI UBORA WA SHULE**
2.1 Uimarishaji wa Mfumo wa Uthibiti Ubora -------------------------------------- 6
2.2 Kuinua Ubora wa Ufundishaji na Ujifunzaji---------------------------------- 7
2.3 Kuboresha Uwazi na Uwajibikaji --------- 7
2.4 Uimarishaji wa Ushirikishwaji wa Jamii -- 8
2.5 Uimarishaji wa Ushirikishwaji, Ujumuishaji na Uhuru -------------------- 8
2.6 Uboreshaji wa Rasilimali ----------------- 9

**11** **SEHEMU YA TATU: UPIMAJI, TATHMINI YA UBORA WA SHULE NA UTOAJI TAARIFA**

3.1 Tathmini ya Ubora wa Shule -----------11
3.2 Utaratibu wa Utoaji Taarifa na Mrejesho--------------------------------14

**17** **SEHEMEU YA NNE: MFUMO WA UENDESHAJI WA UTHIBITI UBORA WA SHULE**

4.1 Utendaji kazi wa Uendeshaji -----------17
4.2 Sifa za Jumla za Watendaji Wakuu-----20
4.3 Maadili ya Mthibiti Ubora wa Shule wa Ndani --------------------------------21

**26** **SEHEMU YA TANO: UFUATILIAJI, TATHMINI NA UJIFUNZAJI KATIKA UTHIBITI UBORA WA SHULE**

5.1 Utangulizi--------------------------------26
5.2 Mwongozo wa Ufuatiliaji wa Tathmini na Ujifunzaji katika Uthibiti Ubora wa Shule ----------------------------------------26
5.3 Ufuatiliaji, Tathmini na Ufundishaji katika Uthibiti Ubora wa Shule----------------27
5.4 Sababu za Ufuatiliaji, Tathmini, na Ujifunzaji katika Mfumo Thabiti wa Uthibiti Ubora wa Shule----------------27
5.5 Mduara wa Ufuatiliaji, Tathmini, na Kujifunza--------------------------------28
5.6 Mduara wa Mradi na Shughuli Zihusianazo na Ufuatiliaji, Tathmini na Ujifunzaji--------------------------------29
5.7 Mchakato faafu wa Ufuatiliaji, Tathmini na Kujifunza katika Mfumo wa Uthibiti Ubora wa Shule -----------------------30

**33** **SEHEMU YA SITA: UTEKELEZAJI WA KIUNZI CHA UTHIBITI UBORA WA SHULE**

6.1 Utangulizi--------------------------------33
6.2 Maeneo Mahususi katika Muongozo wa Utekelezaji Wa Kiunzi cha Uthibiti Ubira wa Shule --------------------------------33
6.3 Usambazaji wa SQAO's-----------------39

**MAREJELEO --------------------------------------------41**




# UTANGULIZI

Dhamira kuu ya jamii na serikali kwa ujumla ni kuhakikisha kuwa elimu inayotolewa inaboreshwa na kudumishwa katika ubora ili kuwawezesha wanafunzi kupata matokeo yaliyokusudiwa. Katika kufanikisha lengo hili kuu, serikali iliunda idara yenye wajibu wa kutathmini shule kote nchini.

Dhamira ya kuwa na mbinu yenye mwelekeo jumuishi na shirikishi kuhusu ubora wa elimu ndio iliyopelekea, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (WyEST) kuhama kutoka kwenye mfumo wa zamani wa Ukaguzi wa Shule kuelekea Mfumo wa Uthibiti Ubora wa Shule kwa kutumia Upimaji wa Jumla wa Shule unaohusisha wadau mbalimbali wakiwemo wanajamii.

Kiunzi cha Uthibiti Ubora wa Shule kilianza kutumika mwaka 2017 kama mbinu ya kufuatilia, kutathmini na kutoa taarifa juu ya viwango vya ubora katika nyanja zote za maisha ya shule ili kuhakikisha kuwa viwango vya ubora vinavyokubalika vinafikiwa na kudumishwa. Baada ya miaka mitano ya matumizi ya awali, ilionekana kuwa ni wakati mwafaka wa kuboresha Kiunzi hicho ili kuchambua utekelezaji wake kwa kuangalia ubora wake, udhaifu, fursa na changamoto zake ili kusaidia kuwa na Kiunzi nyumbufu, kinachoendana na muktadha na jumuishi.

Kiunzi hiki kilichoboreshwa, mbali na kujumuisha elimu ya ufundi kama inavyoelekezwa na Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 (toleo la 2023), kimenuiwa kuwa jumuishi katika azma yake ya kuhakikisha elimu bora kwa wanafunzi wenye mahitaji mbalimbali na wale wa elimu maalum. Kiunzi hiki pia kimefanywa kiendane na masuala ya maendeleo yanayoibuka, matumizi ya teknolojia mpya katika ufundishaji na ujifunzaji na changamoto za kijamii zinazotokana na utandawazi. Changamoto hizi ni pamoja na mmomonyoko wa maadili inayosababishwa na utandawazi, kupotea kwa utamaduni na kupungua kwa uzalendo. Haya yanahitaji kurekebishwa kwa kukuza mtazamo chanya kuhusu utamaduni, kukuza maadili na ujumuishi shuleni ili kufikia ustawi kamili na maendeleo ya wanafunzi.

Kiunzi hiki kitakuwa mwongozo muhimu kwa watathmini elimu, watawala, waendeshaji shule, wamiliki wa shule na wadau wengine wanaohusika katika mchakato na utendaji mzima wa Uthibiti Ubora wa Shule (UUS). Kwa mantiki hii, ni matarajio yangu kuwa wadau wote wanaohusika na UUS watatumia Kiunzi hiki kama mwongozo wa kuboresha viwango vya elimu nchini.

**Mheshimiwa Prof. Aldolf F. Mkenda (Mb)**

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia
Juni, 2024

# SHUKRANI

Nawashukuru kwa dhati wajumbe wa kamati ya ufundi Dkt. Janeth Kigobe, Dkt. Winfrida Malingumu na Dkt. Clarence A. Mgina, pamoja na wataalam wote waliorekebisha tena kiunzi hiki. Pia nawashukuru wakuu wa taasisi mbalimbali, ikiwemo Taasisi ya Elimu Tanzania, Baraza la Mitihani la Taifa la Tanzania, Mamlaka ya Mafunzo na Ufundi Stadi, Tume ya Taifa ya Mafunzo ya Kiufundi na Ufundi, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, Bodi ya Huduma za Maktaba ya Tanzania, na Wakala wa Maendeleo ya Usimamizi wa Elimu; pamoja na wadau muhimu wa elimu, ikiwa ni pamoja na viongozi wa shule, vyuo na wadau wote wa elimu walioshiriki katika kutoa maoni yao na mapendekezo katika mchakato wa kufanyia marekebisho kiunzi hiki.

Kiunzi hiki kimerekebishwa kwa ushirikiano na mashirika mengine, hasa wadau wa maendeleo waliotoa fedha kupitia utendaji wenye mafanikio. Ushiriki wao wa kina umewezesha kupatikana kwa kiunzi hiki chenye viwango na kamilifu katika kuongoza mchakato na shughuli za kuhakiki ubora wa elimu nchini.

Vile vile natambua na kuthamini mchango wa Mhe. Waziri, Prof. Aldolf F. Mkenda (MB) – Waziri wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mhe. Mohamed O. Mchengerwa (MB), wote kwa dhamira yao ya dhati ya kuona kuwa ubora wa elimu ni jambo linalopaswa kuzingatiwa kama lengo kuu katika sekta ya elimu.

**Prof. Carolyne I. Nombo**

Katibu Mkuu,
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
Juni, 2024

## UFAFANUZI **DHANA MUHIMU**

- **Usimamizi kwa Ukaribu:** Ni usimamizi wa utendaji wa wasimamizi wa Shule wa Ndani, hasa kwa kutoa msaada wa kiufundi na kufanya tathmini ya utendaji wa shule kwa ujumla na mara kwa mara. Hii inamaanisha kufanya kazi kwa ukaribu na Wakuu wa Shule ili kutoa elimu bora katika ngazi ya shule. Usimamizi Karibu na Shule utafanywa na Maafisa Elimu Kata, ambao watakuwa na jukumu la kusimamia kila nyanja ya ubora wa elimu katika ngazi ya Kata.

- **Usimamizi wa Nje wa Shule:** Ni usimamizi wa kazi za Wasimamizi wa Ndani wa Shule, na Wasimamizi wa karibu wa Shule na vyombo vingine vyote husika katika ngazi ya Serikali za Mitaa vinavyohusika na usimamizi wa utoaji elimu. Jukumu hili litatekelezwa na Maafisa Uthibiti Ubora kutoka kwenye Wilaya/ Halmashauri, Mikoa na Makao Makuu ya WyEST.

- **Uthibiti Ubora wa Nje wa Shule:** Ni mchakato unaofanywa na Maafisa Uthibiti Ubora wa Shule katika kusaidia shule kuratibu safari yake ya kuelekea kuwa bora kabisa na kuwa na ongezeko la ubora. Hii itahitaji usaidizi katika ufunzaji na unasihi wakati huohuo ikizingatia sera zilizopo, sheria, na kanuni kama zilivyoainishwa katika Sheria ya Elimu na vigezo vya Elimu vya Msingi vya Kitaifa.

- **Usimamizi wa Ndani ya Shule:** Ni usimamizi wa utoaji elimu katika ngazi ya shule unaofanywa na Mkuu wa Shule/Chuo kwa kushirikiana na Timu ya Ndani ya Uthibiti Ubora wa Shule (TNUUS) na Bodi/Kamati ya Shule (BS/KS). Usimamizi ndani ya shule unaiwezesha shule kuwa na uwajibikaji katika nyanja zote za uendeshaji wa shule

- **Uthibiti Ubora wa Ndani ya Shule:** Ni mchakato unaofanywa katika ngazi ya shule na Mkuu wa Shule ili kufuatilia, kutathmini, kuchambua, kufunza, kukuza, na kutoa taarifa viwango vya ubora vilivyokubaliwa katika vipengele vyote vya maisha ya shule ili kuhakikisha viwango vinavyokubalika vinafikiwa na kuendelezwa.

- **Uthibiti Ubora:** Ni programu ya tathmini iliyopangiliwa na kuwekewa utaratibu ili kubainisha uendelezaji na ukuzaji wa viwango vilivyokubalika. Programu hii inakusudia kuwajengea wadau wa elimu hali ya kujiamini kwa kuhakikisha kuwa elimu inatolewa katika viwango vya ubora vinavyokubalika na kwamba wanafunzi wanafikia matarajio ya kujifunza yaliyodhamiriwa.

- **Ukaguzi wa Shule:** Ni shughuli zinazohakikisha kuwa shule inaendeshwa kwa kuzingatia Sheria ya Elimu, Sera, Taratibu na Kanuni zilizopo zinazothibitisha kama shule inaendeshwa kwa usahihi na ufanisi na kutathmini ubora wa shule hiyo kuendana na Viwango vya Kitaifa vya Ubora wa Elimu ngazi ya Elimu ya

Awali, Msingi (za ufundi na za kawaida), Sekondari (za ufundi na za kawaida), Elimu Maalum, Elimu ya Watu Wazima, Elimu Nje ya Mfumo Rasmi, na Elimu ya Ualimu.

- **Tathmini ya Shule:** Ni mchakato endelevu unaowezesha shule kupitia upya utendaji wake na kutambua mafanikio na maeneo yanyohitaji kuboreshwa.

- **Uthibiti Ubora wa Elimu Jumuishi:** Ni mfumo thabiti unaowashirikisha wadau wote husika katika kuhakikisha na kuboresha elimu. Lengo kuu ni kuhusisha kila mtu mwenye jukumu au maslahi katika utoaji wa elimu. Mbinu hii jumuishi inalenga kujenga hisia ya umiliki na uwajibikaji wa pamoja katika kudumisha na kuboresha elimu.

- **Kiunzi cha Uthibiti Ubora wa Shule Nyumbufu:** Ni mwongozo ulioundwa kubadilika kulingana na mazingira ili kukidhi mahitaji maalum na muktadha tofauti za masomo, mazingira, na wanafunzi. Kiunzi hiki kinatambua tofauti zilizopo katika mazingira ya elimu na inalenga kuwa na muundo unaoweza kubadilishwa ili kuendana na muktadha maalum.

- **Ukaguzi wa Utendaji wa Mwalimu:** Ni mfumo wa tathmini ya kina ya utendaji wa walimu ndani ya taasisi ya elimu inayozingatia zaidi ujenzi wa umahiri na uwezo. Mchakato huu unalenga kutathmini na kupima ufanisi wa walimu katika kutimiza majukumu yao, kuhimiza ubora wa ufundishaji na matokeo ya kujifunza wa mwanafunzi.

- **Uthibiti Ubora wa Shule Unaomlenga Mwalimu:** Ni mbinu katika elimu inayosisitiza uboreshaji endelevu wa zoezi la ufundishaji na ubora wa ufundishaji ndani ya shule kwa ujumla wake. Mbinu hii inatambua kuwa ubora wa ufundishaji ni muhimu sana katika mafanikio ya mwanafunzi. Inajumuisha vipengele muhimu na mikakati inayohusiana na maendeleo ya kitaaluma, tathmini ya walimu, msaada na ushauri, ujifunzaji wa pamoja, mifumo ya maoni, maamuzi yanayotokana na takwimu, ushirikiano wa mitaala, uongozi wenye msaada, mgawanyo wa rasilimali, na utamaduni wa uboreshaji endelevu.

- **Uthibiti Ubora wa Shule Unaomlenga Mwanafunzi:** Umejikita katika mahitaji, uzoefu, na matokeo tarajiwa ya elimu ili kumpa mwanafunzi uzoefu bora katika elimu. Mbinu hii inatambua kuwa wanafunzi ni kiini cha mchakato wa elimu, hivyo inalenga kujenga mazingira yanayowasaidia wanafunzi kwa kadri ya mitindo yao ya kujifunza, uwezo, na maendeleo yao kwa ujumla. Katika mbinu hii, uthibiti ubora wa shule unahitaji kuzingatia zaidi wanafunzi na matokeo ya kujifunza yatathmini ushiriki wa wanafunzi katika mchakato wa kujifunza hata wakati mwalimu hayupo. Mbinu hii inaendana na falsafa ya elimu kuwa mwanafunzi ni kitovu cha elimu, hivyo lengo liwe ni kuwawezesha wanafunzi kufikia viwango vya juu vya ubora wao katika mazingira ya elimu wezeshi na jumuishi.

- **Wafanyakazi Wanaotoa Msaada wa Kiufundi:** Ni wafanyakazi wanaotoa msaada wa kiufundi ili kuwezesha utawala kufanikisha taratibu za uendeshaji, ikiwa ni pamoja na usafirishaji, mawasiliano, ununuzi wa vifaa, na kazi za kawaida za ofisi.

# VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| ADEM | Wakala wa Maendeleo ya Usimamizi wa Elimu |
| BSTE-QAF | Kiunzi cha Uthibiti Ubora wa Elimu ya Msingi, Sekondari, na Ualimu |
| CMT | Timu ya Usimamizi wa Chuo |
| DCSQAOs | Maafisa Wakuu wa Uthibiti Ubora wa Shule wa Wilaya |
| DSQAO | Maafisa Uthibiti Ubora wa Shule wa Wilaya |
| DED | Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya |
| DEOs | Maafisa Elimu wa Wilaya |
| DPLA | Upimaji Shirikishi wa Matokeo ya Ujifunzaji |
| ECD | Maendeleo ya Watoto |
| EGMA | Tathmini ya Hisabati katika Daraja la Awali |
| EGRA | Tathmini ya Usomaji katika Daraja la Awali |
| EQUIP-T | Mradi wa Mpango wa Kuboresha Elimu Tanzania. |
| EPforR | Utendaji wenye Mafanikio |
| ESDP | Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Elimu |
| ESMIS | Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Sekta ya Elimu |
| ETP | Sera ya Elimu na Mafunzo |
| FSV | Ziara ya Kufuatilia Shule |
| FYDP | Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano |
| HoSs | Wakuu wa Shule |
| HTs | Walimu Wakuu |
| IAE | Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima |
| ISQATs | Timu ya Uthibiti Ubora wa Ndani wa Shule |
| LANES | Mradi wa kukuza Stadi za Kusoma, Kuhesabu na Kuandika - KKK |
| LGAs | Mamlaka za Serikali za Mitaa |

| | |
|---|---|
| MDA | Wizara, Idara na Mawakala |
| MEWAKA | Mafunzo Endelevu ya Walimu Kazini |
| MoEST | Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia |
| MoHCDGEC | Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto |
| MoW | Wizara ya Maji |
| M & E TWG | Kundi la Kufuatilia na Kutathmini Kazi za Kiufundi |
| NACTVET | Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi |
| NECTA | Baraza la Mitihani la Taifa la Tanzania |
| NEMC | Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira |
| OSHA | Mamlaka ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi |
| PO - RALG | Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) |
| PTA | Chama cha Wazazi na Walimu |
| QA | Uthibiti Ubora |
| QAMA | Mbinu za Usimamizi wa Uhakikisho wa Ubora |
| QS | Viwango vya Ubora |
| RAS | Katibu Tawala wa Mkoa |
| REOs | Maafisa wa Elimu wa Mikoa |
| RSQAOs | Maafisa Uthibiti Ubora wa Shule wa Mkoa |
| RTI | Taasisi ya Utafiti ya Triangle |
| SC/B | Kamati za Shule/Bodi |
| SDGs | Malengo ya Maendeleo Endelevu |
| SMT | Timu ya Usimamizi wa Shule |
| SQA | Uthibiti Ubora wa Shule |
| SQAD | Idara ya Uthibiti Ubora wa Shule |
| SQAH | Mwongozo wa Uthibiti Ubora wa Shule |
| SQAOs | Maafisa Uthibiti Ubora wa Shule |
| SQAS | Mfumo wa Uthibiti Ubora wa Shule |
| SQAT | Timu ya Wathibiti Ubora wa Shule |
| SSQAOs | Maofisa wa Uthibiti Ubora wa Shule wa masomo |
| SSRC | Kadi ya Muhtasari wa Taarifa ya Shule |
| SSV | Ziara Maalum za Shule |

| | |
|---|---|
| SWASH | Mradi wa Huduma za Maji, Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira |
| TCs | Vyuo vya Ualimu |
| TCU | Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania |
| TEA | Mamlaka ya Elimu Tanzania |
| TIE | Taasisi ya Elimu Tanzania |
| ToR | Hadidu za Rejea |
| UNICEF | Mfuko wa Umoja wa Mataifa wa Watoto |
| USAID | Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani |
| VETA | Mamlaka ya Mafunzo na Ufundi Stadi |
| WDC | Kamati ya Maendeleo ya Kata |
| WEOs | Maafisa Elimu wa Kata |
| WSA | Upimaji wa Jumla wa Shule |
| WSDP | Mpango wa Jumla wa Maendeleo ya Shule |
| WSV | Tathmini ya Jumla Shule |



01

SEHEMU YA

# KWANZA

## UTANGULIZI

# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli

Maendeleo ya taifa lolote yanategemea kwa kiasi kikubwa ubora wa elimu inayotolewa kwa wananchi wake. Elimu bora ni muhimu kwa ukuaji wa taifa. Elimu bora ni muhimu kwa kuwapa watu maarifa, ujuzi, na uwezo unaohitajika ili kuchangia kwa ufanisi katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya nchi. Hii pia inaakisiwa na sera za kimataifa, ikiwemo Malengo Endelevu ya Maendeleo (SDGs 2030), hususan Lengo namba 4 linalohusu elimu bora. Aidha, Serikali ya Tanzania imeendelea kuweka na kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuboresha elimu, kama inavyoonesha katika programu mbalimbali, kama vile Maendeleo ya Sekta ya Elimu (ESDP 2022-26), ambayo lengo lake ni kujenga uchumi shindani wa viwanda kwa maendeleo ya binadamu.

Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 (toleo la mwaka 2023), imeeleza kwa kina suala la Uhakiki wa Ubora wa Elimu na Mafunzo na kusisitiza kwamba lengo lake ni kuwa na ufanisi katika uratibu, usimamizi, uthibitishaji, na ukaguzi katika kutoa elimu na mafunzo.

Kulingana na tamko la Sera, Wizara inayohusika na elimu na mafunzo inawajibu wa kufuatilia ubora wa shule katika ngazi zote kulingana na mitaala na viwango vilivyowekwa. Hata hivyo uthibiti ubora wa elimu ya awali, elimu ya msingi, elimu ya sekondari, na elimu ya ualimu inayoratibiwa na Idara ya Uthibiti Ubora wa Shule imeendelea kukabiliana na changamoto mbalimbali na hivyo kushindwa kukidhi matarajio. Licha ya kutumia dhana ya uthibiti ubora wa shule shirikishi na matumizi ya njia mbadala, changamoto imeendelea kuwa muendelezo wa dhana ya ukaguzi wa shule inayojikita zaidi katika kupitia orodha ya masuala yanayohitaji kufanywa katika ufundishaji na ujifunzaji. Hivyo, bado ipo haja ya kuimarisha utekelezaji wa dhana iliyokusudiwa ya uthibiti ubora inayojikita katika ushirikishwaji na uwajibikaji wa pamoja wa Kamati na bodi za shule/vyuo, walimu wakuu wa vyuo vya mafunzo ya elimu ya msingi, viongozi wa shule, walimu, waalimu wa mafunzo, wakufunzi pamoja na wazazi katika suala la usimamizi na uthibiti wa ubora wa elimu inayotolewa nchini. Ndiyo maana, katika kutilia mkazo suala hili la uthibiti ubora wa elimu, serikali imetoa tamko namba; 3.3.1, 3.3.2, 3.3.3 na 3.3.4 katika Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 (toleo la mwaka 2023).

Katika kutekeleza maagizo haya ya sera, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, kupitia Idara ya Uthibiti Ubora wa Shule, imeendelea kusimamia ubora wa elimu kwa kuhakikisha kwamba wadau wa elimu na taasisi zote katika ngazi ya elimu

ya awali, msingi (za ufundi na kawaida), sekondari (za ufundi na za kawaida) na vyuo vya walimu wanazingatia Sera, Sheria, Kanuni, Miongozo na viwango vya ubora vya elimu vilivyowekwa. Nyenzo kuu inayotumiwa ni Kiunzi cha uthibiti ubora ulioandikwa mwaka 2017 na zana zake, ambazo ni pamoja na Mwongozo wa Uthibiti wa Ubora Ulioambatanishwa, Mwongozo kwa Maafisa Elimu wa Wilaya na Kadi ya Muhtasari wa Taarifa ya Shule. Kiunzi na zana zake kimewezesha ufuatiliaji, tathmini na utoaji wa taarifa kuhusu vigezo vya ubora vilivyokubaliwa kuhusu masuala yote yanayohusiana na maisha ya shule ili kuhakikisha viwango vya ubora vinakidhiwa na kuendelezwa na hivyo kuonyesha mafanikio makubwa katika kusimamia ubora wa elimu. Kulingana na mafanikio haya, Wizara imeona umuhimu wa kupitia kiunzi hiki baada ya miaka mitano ya matumizi ili kiendane na mahitaji ya sasa ya Sera na mtaala ulioboreshwa, ambayo kimsingi yanalenga kuleta mageuzi katika mfumo mzima wa elimu na mafunzo.

Kiunzi hiki kinatarajiwa kuwa nyumbufu, kuendana na mazingira na jumuishi kwa masomo na viwango mbalimbali, kutokana na kutambua kwamba stadi tofauti zinaweza kuwa na mahitaji na vigezo tofauti vya tathmini. Kiunzi kinapaswa kuweka viwango vya wazi na vinavyoweza kupimika na matokeo ya kujifunza ambayo yanaweza kubadilishwa kulingana na masomo na mazingira ya elimu tofauti na kufafanua vigezo vya mafanikio vinavyoweza kutumika katika nidhamu mbalimbali.

Kulingana na kiunzi hiki, wigo na majukumu ya msingi ya Mfumo wa Uthibiti Ubora wa Shule imepanuliwa ili kujumuisha wahusika muhimu kama vile wizara zinazohusika na usimamizi na utawala wa elimu na taasisi zao, Maafisa Uthibiti Ubora wa Shule, Maafisa wa Elimu wa Mikoa, Maafisa wa Elimu wa Wilaya, Maafisa wa Elimu wa Kata, Wathibiti Ubora wa Ndani ya Shule, walimu, wazazi, na jamii ambao watakuwa wanashiriki kikamilifu katika kukuza ubora katika mchakato wa utoaji wa elimu. Kwa muktadha huu, Kiunzi cha Uthibiti Ubora wa Shule kitafanya kazi kwa kufuata dira ya ujumuishaji ambao unakuza mawasiliano yenye ufanisi kati ya wizara, taasisi, uwazi, na uamuzi wa pamoja kuhusu masuala ya uthibiti ubora wa elimu.

## 1.2 Dira na Dhima ya Elimu

Dira na Dhima ya Elimu kama ilivoelezwa katika Dira ya Maendeleo ya Tanzania ya 2025 inatoa mwongozo kuhusu utoaji wa elimu bora.

### 1.2.1. Dira

Kuwa na Mtanzania aliyeelimika, mwenye maarifa, stadi na mtazamo chanya utakaomwezesha kuchangia katika kuleta maendeleo endelevu ya Taifa.

### 1.2.2. Dhamira

Kuinua ubora wa elimu na mafunzo kwa kuweka mifumo na taratibu zitakazowezesha kupata idadi kubwa ya Watanzania walioelimika, wenye stadi na wanaopenda kujiendeleza kielimu ili waweze kuchangia katika kufikia malengo ya maendeleo ya Taifa.

Matamko ya dira na dhima ya elimu ni viashiria vya dhamira ya Serikali ya kutoa elimu bora kwa wote na stadi za kazi kwa Watanzania wote. Kwa mantiki hii, Kiunzi hiki kinaakisi matamko ya Dira na Dhima.

## 1.3 Urazini

Pamoja na mafanikio yaliyobainishwa wakati wa utekelezaji wa Kiunzi cha Uthibiti Ubora wa Shule, changamoto kadhaa zimejitokeza kutokana na mfumo na njia zilizotumika katika kuhakiki ubora wa elimu. Kwa mfano, kumeonekana haja ya kuwa na vigezo muhimu zaidi vya kutathmini elimu ya awali, elimu maalum, elimu ya ualimu, elimu ya watu wazima, na elimu isiyo rasmi. Pia, ukosefu wa vigezo na viashiria vya kutosha vya ubora kwa kila nyanja ulipelekea kuwa na matokeo ya jumla kuhusu ubora wa shule. Udhaifu pia ulionekana katika kukosekana kwa mawasiliano baina ya wizara juu ya maamuzi mbalimbali yanayolenga kuhakiki ubora. Matokeo yake, kazi moja ilifanywa na wadau mbalimbali, na hivyo kusababisha urudiaji wa jambo moja na ucheleweshaji wa maamuzi muhimu. Upungufu huu ulileta changamoto katika utekelezaji wa mfumo na ufikiaji wa matokeo tarajiwa. Zaidi ya hayo, marekebisho yaliyofanywa kwenye mitaala ya elimu ya msingi na sera ya elimu pia yamechagiza urekebishaji wa Kiunzi cha uthibiti ubora wa shule.

Kwa hiyo, upitiaji upya na mapendekezo ya marekebisho ya kiunzi yanakusudia kuboresha dhana, mfumo, njia, na falsafa ya Idara ya Uthibiti Ubora wa Shule ili iendane na mahitaji halisi ya sasa na ya mtalaa mpya katika ngazi ya elimu ya awali, elimu ya msingi (za kawaida na za ufundi), elimu ya sekondari (za kawaida na za ufundi), elimu ya ualimu, na elimu isiyo rasmi. Wakati huo huo, inapaswa kuwa jumuishi na toshelezi kwenye miktadha maalum, masomo, mazingira, na wanafunzi tofauti. Kiunzi hiki kitatambua tofauti zilizopo katika mazingira ya elimu na kutoa muundo unaoweza kubadilishwa kulingana na hali mahususi.

Hususani, kiunzi kimeboreshwa ili iweze:

i. Kuendana na muundo ulioboreshwa wa Idara ya Uthibiti Ubora wa Shule ambao unakwenda sambamba na matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika kutekeleza majukumu ya kuhakiki ubora na mifumo ya usimamizi wa data.
ii. Kuweka viashiria vya ubora katika maeneo yote.
iii. Kurahisisha tathmini inayohusisha elimu ya awali, elimu maalum, elimu ya watu wazima na elimunje ya mfumo rasmi na elimu ya ufundi.
iv. Kuweka vigezo na viashiria vya ubora kwa taasisi za kifani na kiufundi.
v. Kutoa zana sahihi kwa matumizi na taasisi zinazotoa elimu ya mchanganyiko.
vi. Kumwongoza mtumiaji jinsi ya kutekeleza majukumu yake kikamilifu kina na kiweledi.
vii. Kuhamasisha mawasiliano na ushirikiano baina ya wizara na taasisi.
viii. Mapitio ya mfumo wa uthibiti ubora wa shule yanaakisi mabadiliko ya lazima yaliyofanywa ili kuendana na mtalaa na sera ya elimu iliyorekebishwa

## 1.4 Lengo

Lengo la Kiunzi hiki ni kuwapatia wadau wanaohusika na Uthibiti Ubora wa elimu mikakati, taratibu, na miongozo iendayo sambamba na Kanuni na Viwango vya Elimu kwa ajili ya kuinua ubora wa elimu na matokeo ya ujifunzaji katika ngazi za Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari, Elimu Maalum, Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi na Elimu ya Vyuo vya Ualimu nchini Tanzania.

## 1.5 Mawanda

Kiunzi hiki kitatumika kama mwongozo wa kusimamia masuala ya ubora wa elimu kwa ngazi za Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari, Elimu Maalum, Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi na Elimu ya Ualimu. Kupitia Kiunzi hiki, Wathibiti Ubora wa Shule, wamiliki wa shule, watawala na waendeshaji wa Shule, Maafisa Elimu (ngazi za Mkoa, Halmashauri/Wilaya na Kata), Wakuu wa Shule/ Walimu Wakuu, Wakuu wa Vyuo, Wakufunzi, Walimu, Wazazi, Wanafunzi na jamii kwa ujumla watapata mwongozo wa namna ya kufanya shughuli za Uthibiti Ubora katika maeneo yao ya kiutendaji.

02

SEHEMU YA

# PILI

## KANUNI NA TARATIBU ZA UTHIBITI UBORA WA SHULE

## KANUNI NA TARATIBU ZA UTHIBITI **UBORA WA SHULE**

Sehemu hii inaeleza kanuni na taratibu za Uthibiti Ubora wa Shule. Maelezo haya yametokana na uelewa na namna matokeo ya ujifunzaji yatakavyo tathminiwa na kuboreshwa Kwa hiyo, uboreshaji wa matokeo ya ujifunzaji kimsingi unahusisha vipaumbele nane muhimu, ambayo ni pamoja na: uimarishaji wa Mfumo wa Uthibiti Ubora wa Shule, uboreshaji wa rasilimali (utoaji wa vifaa, rasilimali watu, fedha, na vifaa vya kutosha), uboreshaji wa ufundishaji na ujifunzaji, kuongeza uwazi na uwajibikaji, kuchagiza ushirikishwaji, tofauti, na mabadiliko, kujikita kwenye maarifa na umahiri wa mwanafunzi, kukuza uboreshaji endelevu na kuongeza ushirikishwaji wa jamii, kama ilivyowasilishwa kwenye **Kielelezo Na. 1.**




Mwongozo na zana za Utendaji wa Uthibiti Ubora zimesanifiwa mahsusi ili kubeba vipaumbele vitano kama vilivyofafanuliwa kwenye sehemu ya 2.1 hadi 2.8.

### 2.1 Uimarishaji wa Mfumo wa Uthibiti Ubora

Mfumo wa Uthibiti Ubora utaimarishwa katika nyanja zote ili kuhakikisha utekelezaji wa ufanisi na wenye tija wa sera za elimu, sheria, na kanuni ili kutoa elimu bora. Lengo la kuimarisha mifumo ya Uthibiti Ubora katika nyanja zote

inahusisha mbinu zote ikiwemo ujenzi wa uwezo, kushirikishana habari, uongozi na usimamizi, usimamizi, ufuatiliaji na tathmini, na ufuataji wa viwango vya kitaifa. Mkakati mzima huu unalenga kuunda mfumo imara wa kutoa elimu bora kwa kuzingatia sera na kanuni zilizowekwa. Vipengele muhimu katika kuimarisha Mfumo wa Uthibiti Ubora ni pamoja na uboreshaji wa mfumo wa uthibiti ubora wa ndani, usimamizi karibu na shule, uthibiti ubora wa nje, mfumo wa habari na mawasiliano, kuajiri wafanyakazi kwa kuzingatia sifa zao, bila kujali tofauti zao na bila ubaguzi, na kwa kufuata vigezo vya kuajiri na kupeleka waajiriwa sehemu za kazi. Vipengele vingine ni pamoja na kuwezesha mazingira, kama vile kusaidia shughuli za ofisi kuendelea, miundombinu, na kanuni za maadili na utunzaji wa siri. Maelezo ya kina kuhusu mambo haya yatatolewa katika Mwongozo wa Uthibiti Ubora wa Shule, mwongozo wa uendeshaji, na miongozo mingine. Zana nyingine zitatengenezwa kulingana na Kitabu cha Uthibiti Ubora na Mwongozo wa Uendeshaji ili kufuatilia na kutangaza matokeo. Zana hizo zitajumuisha Kitabu cha Kumbukumbu, Fomu ya Kujitathimini za Shule, Kadi ya Taarifa za Shule, na Mwongozo wa Mafunzo.

## 2.2 Kuinua Ubora wa Ufundishaji na Ujifunzaji

Katika kuboresha ufundishaji na ujifunzaji, Uthibiti Ubora utajikita katika kubainisha, kufafanua, na kutathmini viashiria vya kufanyika kwa ufundishaji na ujifunzaji, michakato, pamoja na matokeo ya ujuzi na ufanisi ili kuhakikisha uboreshaji wa utendaji kulingana na viwango vya elimu vilivyowekwa. Hususani, viashiria vya mahitaji, michakato, na matokeo yataendelezwa kulingana na muhtasari wa masomo (mikataba, vitabu vya kiada, miongozo kwa walimu, moduli, na tathmini ya wanafunzi inayotegemea ufanisi) na ujuzi uliokuzwa na wanafunzi. Mkazo uwekwe katika kulinganisha muhtasari wa masomo na malengo na viwango vya elimu. Uundaji au uigizaji wa zana za tathmini za utambuzi na ufuatilijia ambazo zinaweza kutoa matokeo endelevu juu ya zoezi la kufundisha na kujifunza ya walimu na ujifunzaji wa wanafunzi. Tathmini za maendeleo zitatumika kubaini zoezi halisi la kufundisha na kujifunza yanayotokea darasani na kwa kutumia mbinu hii, malengo, na viwango vitawekwa. Viashiria vya utendaji na tathmini endelevu vitasaidia zaidi kwenye njia shirikishi ya kuboresha matokeo ya kufundisha na kujifunza. Uthibiti Ubora wa Shule pia inapaswa kutumia taarifa za tathmini kupima ufanisi wa mbinu za kufundisha ili kutambua maeneo ya kuboresha. Kiunzi cha Uthibiti Ubora wa Shule kitasisitiza thamani ya maarifa na ufanisi wa wanafunzi kwa kukuza mikakati mbalimbali ya tathmini, ikiwa ni pamoja na tathmini za kufuatilia maendeleo na tathmini ya mwisho, ili kupima maarifa na ujuzi wa mwanafunzi.

## 2.3 Kuboresha Uwazi na Uwajibikaji

Uwazi na uwajibikaji utaboreshwa kwa kujenga ufahamu juu ya shughuli za Mfumo wa Uthibiti Ubora ili kurahisisha ripoti za uthibiti ubora na Kadi ya Muhtasari wa Taarifa ya Shule. Taarifa hizi zitaandaliwa na kutolewa kwa wadau wote muhimu kwa uwazi, ikiwa ni pamoja na Taasisi ya Elimu Tanzania, Baraza la Mitihani Tanzania, Baraza la Kitaifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (wakurugenzi watendaji wa wilaya, makatibu tawala wa mikoa, maafisa elimu wa mikoa, maafisa elimu wa wilaya, na maafisa elimu

wa kata), walimu, wazazi, wanajamii, na washirika wa maendeleo; hii inakwenda sambamba na kuelezea majukumu yao na wajibu. Kwa hiyo, maofisa uthibiti ubora wa shule katika ngazi zote watajengewa uwezo katika mawasiliano na kuandika taarifa. Vilevile, miongozo ya kuajiri na kupangia vituo wahakiki ubora, wakuu wa mikoa na wilaya, maafisa elimu wa mkoa, maafisa elimu wa wilaya, maafisa elimu wakata, wakuu wa shule, na wakuu wa shule itaundwa. Pia, miongozo ya mafunzo na zana sahihi itaelezea majukumu na wajibu wa wahusika muhimu katika viwango tofauti. Kiunzi cha uthibiti ubora kinapaswa kuendeleza mfumo imara wa mrejesho, ambayo itatoa maoni yenye tija kwa shule, walimu, na wanafunzi na hivyo kuwezesha matumizi ya taarifa za uthibiti ubora wa shule kusaidia ufanyaji wa maamuzi ya ufundishaji na uboreshaji mitaala. Hii inaweza kufanywa kwa kuchambua matokeo ya tathmini mara kwa mara ili kubaini mwelekeo, mapengo, na maeneo ya kuboresha. Hii inawezesha kujenga mfumo wa uthibiti ubora wa kisasa na unaoweza kubadilika kulingana na wakati katika kuinua kiwango cha ufundishaji kwa taasisi zote.

## 2.4 Uimarishaji wa Ushirikishwaji wa Jamii

Ushirikishwaji wa jamii ni kipengele muhimu katika kusaidia utoaji wa elimu bora. Hivyo, ushirikishwaji wa jamii husaidia kufanikisha uthibiti ubora wa shule. Kwa kuzingatia hili, ushirikishwaji wa jamii utaimarishwa kwa kuunda majukwaa yanayowezesha kuwepo kwa mahusiano kati ya wahusika muhimu wa uthibiti ubora wa shule na jamii. Mfano wa jukwaa kama hiyo ni Mpango wa Kuboresha Shule, ulioundwa kwa kushauriana na jamii na wadau wengine kama wathibiti Ubora, Timu ya Usimamizi wa Shule, na maafisa elimu kata ili kushughulikia masuala ya ubora wa elimu. Hii itafanywa ili kuhakikisha jamii inasaidiwa, inashirikishwa, na inamilikishwa Wathibiti Ubora wa Shule, na hivyo kuboresha shule.

## 2.5 Uimarishaji wa Ushirikishwaji, Ujumuishaji na Uhuru

Kuchochea ushirikishwaji wa jamii na makundi tofauti tofauti katika uthibiti ubora hujumuisha kuhakikisha kuwa michakato na mifumo imeundwa kwa njia inayofaa, yenye uwiano, na inayojibu mahitaji ya wanafunzi mbalimbali. Mfumo wa Uthibiti Ubora wa Shule unapaswa kuhakikisha kuwa timu za uthibiti ubora zina wawakilishi kutoka kwa kundi la wanafunzi kulingana na idadi yao shuleni. Pia, mfumo wa Uthibiti Ubora wa Shule unapaswa kuhakikisha kuwa vifaa vya muhtasari wa masomo na rasilimali vinaakisi mitazamo mbalimbali na vinajali tamaduni, na vile vile zinakuza utamaduni wenye kuthamini na kuheshimu kila mtu kwa jinsi alivyo.

Kuhusu uhuru, Mfumo wa Uthibiti Ubora wa Shule utazingatia mahitaji maalum ya masomo, viwango vya elimu, mahitaji na umri wa wanafunzi, muktadha wa taasisi, na vipengele vya maarifa na umahiri unaotegemewa katika kujifunza. Kufanikisha hili, wafanyakazi wanaohusika na Uthibiti Ubora wanapaswa kuwa na ujuzi, umahiri wa utamaduni, uelewa juu ya ushirikishwaji, na ufahamu wa makundi tofauti za wanafunzi ili kutambua na kuhakiki upendeleo wowote katika tathmini ya ubora wa elimu.

## 2.6 Uboreshaji wa Rasilimali

Upatikanaji na utoshelevu wa rasilimali utakuwa sehemu muhimu ya viashiria vya ubora. Hata hivyo, uthibiti wa upatikanaji halisi, utoshelevu, na matunzo ya rasilimali zinazoonekana kama ofisi, vyombo vya usafiri, samani, vifaa vya elektroniki na programu, majengo muhimu, na vifaa vya kufundishia na kujifunzia, pamoja na bajeti katika viwango tofauti, utaamuliwa na wizara husika na wamiliki wa shule. Kwa hiyo, wahusika muhimu katika ngazi zote watahakikisha rasilimali za kutosha zinahamasishwa na kutumika kuhakiki ubora kwa ufanishi katika elimu ya msingi, sekondari, ualimu, na katika mfumo wa elimu usiyo rasmi.

Uhamasishaji wa rasilimali utajumuisha kuajiri na kupeleka idadi inayotosha ya Maafisa Uthibiti Ubora wa Shule wenye sifa, ujuzi, na uwezo katika ngazi za taifa, kanda, na wilaya. Kitajumuisha pia kukuza na kutekeleza programu endelevu ya kujenga uwezo kwa maafisa elimu wa mkoa, maafisa elimu wa wilaya, na maafisa elimu wa kata, na wakuu wa shule; juu ya Kiunzi cha Uthibiti Ubora wa Shule ili kuboresha uwezo wao. Kutakuwa pia programu endelevu za kujenga uwezo, umahiri, uwajibikaji na morali katika ngazi zote kwa walimu tarajali na wale walioko makazini. Hata hivyo, hili litaweza kufanikiwa tu ikiwa bajeti zinazohitajika na Idara ya Uthibiti Ubora zitapangwa na idara husika na ikiwa itapewa mamlaka ya kuadhibu watendaji/wafanyakazi wasio na ufanisi.

Kuhusu rasilimali vitu, wathibiti ubora wa shule katika ngazi zote watahakikisha kuwa wananunua bidhaa zinazoendana na thamani ya pesa waliotoa na kufuatilia huduma za usimamizi wa fedha na uhasibu kwa kuwapa semina maafisa wa uhasibu ili wawe na ujuzi, uwezo, maadili, uzalendo, uwajibikaji, na uwajibikaji.

Muda utasimamiwa kwa kuelezea wazi majukumu, muda, na mipango ya uthibiti ubora wa shule katika ngazi ya kitaifa, kikanda, wilaya, kata, na shule ili kutekeleza shughuli za Uthibiti ubora wa Shule katika ngazi zote bila kuhatarisha ustawi wa wafanyakazi..



03

SEHEMU YA
# TATU

# UPIMAJI, TATHMINI YA UBORA WA SHULE NA UTOAJI TAARIFA

## UPIMAJI, TATHMINI **YA** UBORA WA **SHULE NA UTOAJI TAARIFA**

Upimaji na tathmini ya Ubora wa Shule utalenga kwenye ufanisi wa shule katika nyanja mbalimbali kama vile; ubora wa mitaala katika kukidhi mahitaji ya mwanafunzi, ubora wa ufundishaji kwa ujifunzaji na upimaji mzuri, ubora wa uongozi na uendeshaji (uongozi katika ujifunzaji, uongozi wa watu na rasilimali), ubora wa mazingira ya shule na athari zake kwenye ustawi, afya na usalama wa wanafunzi, ushirikishwaji wa jamii, maadili, utamaduni na uzalendo, matumizi bora ya habari, mawasiliano na teknolojia na mafanikio ya wanafunzi,

## 3.1 Tathmini ya Ubora wa Shule

### 3.1.1 Ubora wa Mtaala katika kukidhi Mahitaji ya Wanafunzi

Uwanja huu utalenga kwenye masuala ya upatikanaji, umaana, na matumizi ya vifaa vya mtaala pamoja na uzingatiaji wa viwango vya ubora wa mtaala. Wathibiti Ubora wa Shule, pia watahakikisha kama mipango ya utekelezaji wa mtaala wa shule ni jumuishi na inajumuisha masuala mtambuka ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi yanayotofautiana

### 3.1.2 Ubora wa Ufundishaji kwa Ujifunzaji na Upimaji Mzuri

Kwa kutumia Uwanja huu, Uthibiti Ubora wa Shule utajikita katika kutathmini matumizi fanisi ya mbinu za ufundishaji zinazomlenga mwanafunzi, usahihi na matumizi ya maandalio ya masomo, vifaa na zana za kufundishia na kujifunzia, uelewa wa walimu kuhusu mahitaji ya wanafunzi, ufahamu wa walimu kwenye masomo na upimaji wa matokeo ya ujifunzaji.

Mkazo katika eneo hili utawekwa kwenye kutathmini walimu na wakufunzi ili kuhakikisha kuwa wanatumia vifaa vya kufundishia vyenye ubora wa hali ya juu na kuunda mazingira ya kujifunza yanayoendana na kiwango cha elimu wanachofundisha na muktadha wa taasisi yao. Eneo hili litazingatia mambo kama uwezo wa mwezeshaji, ubora wa ufundishaji, njia na mikakati ya kufundisha, usimamizi wa darasa, tathmini na maoni, maendeleo ya kitaaluma, ushirikiano na mawasiliano, ushiriki wa wanafunzi, maadili ya kitaaluma na matokeo. Zaidi ya hayo, walimu wanapaswa kutoa mrejesho kwa wanafunzi na kuwahamasisha.

### 3.1.3 Ubora wa Uongozi na Utawala: Uongozi wa Ujifunzaji, Watu na Rasilimali

Katika eneo hili, tutajikita katika kutathmini ubora wa uongozi na usimamizi kwa kuzingatia nyanja ya Mabadiliko na Ubunifu, Uongozi na Usimamizi wa Watu na Rasilimali, na Uongozi wa ujifunzaji.

#### 3.1.3.1 Mabadiliko na Uvumbuzi

Katika kipengele hiki, tathmini itajikita katika ukaribu na wakuu wa shule au utoaji wa muongozo wa wazi ya muelekeo wa elimu kwa viongozi wa shule na kiwango ambacho nyaraka za mipango mkakati wa shule zinafanyiwa marekebisho na kutawanywa kwa wanajamii wa shule. Pia, tutajikita kwenye umahiri na ubunifu wa walimu na viongozi kwenye mahitaji ya kisheria juu ya mitaala, afya na usalama, na usimamizi wa wafanyakazi.

#### 3.1.3.2 Uongozi na Usimamizi wa Watu na Rasilimali

Uongozi na Usimamizi wa Rasilimali watu na rasilimali ni muhimu katika kufikia malengo ya Uthibiti Ubora wa Shule. Kwa kuzingatia hili, tathmini itazingatia kiwango ambacho viongozi wa shule wanavyoendeleza na kukuza uhusiano wa kikazi kati ya wafanyakazi na kuhakikisha kuwa kuna utekelezaji mzuri na uwajibikaji. Aidha, tathmini itazingatia utekelezaji mzuri na uwajibikaji na jinsi viongozi wanavyodhihirisha ubunifu na uwezo katika kutumia rasilimali zilizopo kuboresha matokeo ya kujifunza, uwazi, na ufikiaji maamuzi..

#### 3.1.3.3 Uongozi wa Ujifunzaji

Katika kipengele hiki, tathmini itajikita katika kuangalia kiwango ambacho wakuu wa shule na vyuo wana uelewa wa ubora wa mitaala, viwango vya ubora katika ufundishaji, ujifunzaji, na tathmini, na kama viongozi hawa wanakutana mara kwa mara na walimu/wakufunzi kujadili matokeo ya tathmini. Vile vile, tathmini itahakikisha kuwa wakuu wa shule na vyuo wanatembelea mara kwa mara madarasa na kufuatilia ufundishaji na ujifunzaji na kutoa maoni yenye kujenga kwa walimu/wakufunzi. Aidha, Maafisa Uthibiti Ubora wa Shule watazingatia kiwango ambacho wakuu wa shule na vyuo wanawatia moyo walimu kujifunza kutoka kwa wenzao na kutumia maarifa yao kuboresha matokeo tarajiwa ya kujifunza. Pia, wanapaswa kuwa na uwezo wa kuwaalika wataalamu kutoka nje ya shule kuelezea viwango bora vinavyotakiwa, na kuandaa ziara za uwandani, na kuhamasisha matumizi ya teknolojia katika kujifunza ili kuboresha matokeo tarajiwa ya kujifunza.

### 3.1.4 Ubora wa Mazingira ya Shule na Matokeo Yake katika Ustawi, Afya na Usalama wa Wanafunzi

Mazingira ya shule yanachangia sana kufikia matokeo tarajiwa ya kujifunza kwa wanafunzi. Kwa hiyo, katika nyanja hii, tathmini iangalie ikiwa wanafunzi wanapata msaada unaowawezesha kuendeleza na kudumisha mtindo wa maisha wenye afya na usalama, na kujua kiwango ambacho shule inavyotumia motisha kukuza ujifunzaji. Pia, tathmini ijikite katika kuangazia jinsi shule inavyofuata sheria za kitaifa na za shule, kanuni, na masuala ya kupangiwa kazi wafanyakazi. Mazingira pia yanapaswa kukuza masuala ya kiakili, kimwili, kijamii, kiroho, na masuala mengine mtambuka.

### 3.1.5 Ushirikishwaji wa Jamii

Katika kipengele hiki, tathmini itazingatia ikiwa shule/vyuo vya maendeleo ya wananchi/chuo na shule huria zinashirikisha na kushirikiana na jamii; ikiwa jamii iko tayari kushiriki na kuchangia katika Mpango wa Jumla wa Maendeleo ya

Shule; ikiwa shule na jamii wanashirikiana kwa kiasi kikubwa katika kutoa taarifa za kuboresha shule; na ikiwa shule inajenga ushirikiano na jamii ili kuboresha kujifunza..

### 3.1.6 Maadili, Utamaduni na Uzalendo

Mfumo wa Uthibiti Ubora wa Shule kwa kawaida hujumuisha vipengele mbalimbali ili kuhakikisha taasisi za elimu zinadumisha viwango vya juu na kutoa uzoefu mzuri katika kujifunza. Maadili ni sehemu muhimu ndani ya mfumo huu kutokana na mchango wake katika utoaji wa elimu bora kwa ujumla.

Upimaji wa maadili unahitaji mbinu mtambuka zinazozingatia vigezo vya kiasi na ubora. Uundaji wa utamaduni wa shule unaochechea maadili, na uzalendo katika kufikia maadili ni muhimu. Marekebisho ya mara kwa mara ya njia za tathmini yatasaidia kuboresha daima kipengele hiki muhimu cha uthibiti ubora wa shule. Kipengele cha maadili na katika mfumo wa uthibiti ubora wa shule kinazingatia kuunda utamaduni chanya, wa maadili, na jumuishi shuleni; na unalenga kusaidia ustawi na maendeleo ya wanafunzi kwa ujumla.

Kuhusu utamaduni na uzalendo, ni muhimu kuelewa kuwa utandawazi, tofauti za kiuchumi, na mwingiliano wa watu kutoka tamaduni tofauti vimechangia mabadiliko katika maadili na tabia, na hivyo kuleta changamoto mbalimbali katika jamii. Kwa kuwa elimu katika taifa ni msingi wa kudumisha amani ya kijamii kwa kujenga ujuzi wa kutatua migogoro, umoja wa kijamii, na mshikamano, inapaswa kuwa imara kuwawezesha watanzania kuelewa, kulinda, na kukuza misingi ya maadili na uadilifu wa kitaifa, ikiwa ni pamoja na utu, uzalendo, umoja, uwazi, uaminifu, uwajibikaji, pamoja na kuthamini haki za kiraia na wajibu wao.

### 3.1.7 Matumizi Bora ya Taarifa, Mawasiliano na Teknolojia

Kuhusu matumizi ya teknolojia katika Uthibiti Ubora wa Shule, lengo ni kutathmini jinsi Teknolojia ya Habari, Mawasiliano, na Teknolojia inavyohusishwa katika nyanja mbalimbali za mchakato wa elimu ili kuboresha ufundishaji, ujifunzaji, na usimamizi wa shule kwa ujumla. Hii pia ni pamoja na ujifunzaji mtandaoni na madarasa bora. Kwa sababu ya maendeleo haya katika matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano, shule/walimu wanapaswa kubadilisha njia zao ya kutekeleza mitaala kwa kutumia teknolojia ya mfumo wa habari katika mchakato wa kujifunza.

### 3.1.8 Mafanikio ya Mwanafunzi


Kutathmini mafanikio ya utendaji wa wanafunzi ni sehemu muhimu ya uthibiti ubora wa shule kutokana na kuwa kunatoa taarifa muhimu kuhusu ufanisi wa programu za elimu na husaidia kutambua maeneo yanayohitaji kuboreshwa. Ni muhimu kutumia njia anuwai za tathmini katika kipengele hiki ili kuelewa mafanikio ya wanafunzi kwa kina. Kutathmini mafanikio ya wanafunzi ndani ya Mfumo wa Uthibiti Ubora wa Shule unaoweza kubadilika kunahusisha njia tofauti kwa kuzingatia mambo mbalimbali. Mbali na matokeo ya tathmini kama vile mitihani ya kila wiki, kila mwezi, mwisho wa muhula, mwaka, na mitihani ya kitaifa, eneo hili linapaswa kutathminiwa kwa kutumia taarifa zinazotokana na ujifunzaji halisi darasani, mazoezi ya vitendo nje na ndani ya eneo la shule, na tathmini ya

uwezo wa wanafunzi kutumia taarifa na kufanya baadhi ya majukumu. Uwezo wa wanafunzi, ubunifu, na mabadiliko ya tabia pia yanapaswa kuongoza Uthibiti Ubora wa Shule katika kutathmini kujifunza bila kujali uwezo wa wanafunzi kulingana na viwango vyao..

## 3.2 Utaratibu wa Utoaji Taarifa na Mrejesho

Katika mchakato mzima wa Upimaji na Tathmini ya Ubora wa Shule, utaratibu wa utoaji taarifa, mrejesho, na ufuatiliaji ni muhimu sana kwa uwepo wa mawasiliano fanisi kwenye Mfumo wa Uthibiti Ubora. Kielelezo Na. 2 kinaonesha mchakato mzima wa uthibiti ubora wa shule na ufuatiliaji unavyofanyika.

Kielelezo Na. 2: Utaratibu wa Utoaji Taarifa ya Uthibiti Ubora wa Shule na Ufuatiliaji




Ofisi ya Uthibiti Ubora wa Shule itapewa jukumu la kufanya mawasiliano wakati wowote kutoa taarifa ya uthibiti ubora wa shule moja kwa moja kwa wadau wote wanaohusika katika wizara mama (yaani Wizara ya Elimu Sayansi na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa) na taasisi zake zote zinazohusika na suala la uthibiti ubora. Pia, nakala za taarifa hizo zitapelekwa kwenye halmashauri husika, wamiliki na mameneja wa shule, wazazi, maafisa elimu kata, na wakuu wa shule na vyuo. Kuna njia tofauti za kutoa taarifa kama vile magazeti, tovuti, mtandao, televisheni na redio, vifaa vilivyochapishwa kama vipeperushi, mabango, Kadi ya Muhtasari wa Taarifa ya Shule, na vijitabu. Pia, mikutano ya kusambaza taarifa itafanyika ili kuongeza ushiriki mpana, uwazi, na uwajibikaji katika ngazi zote. Aina ya taarifa, muundo, na wapokeaji itategemea aina ya tathmini ya shule iliyoelekezwa katika Mwongozo na Kiunzi cha Uthibiti Ubora wa Shule. Kwa hivyo, mfumo wa kutoa taarifa na kutoa maoni kwa ufanisi utahitaji Maafisa Uthibiti

Ubora wa Shule na wahusika muhimu wa elimu kuhakikisha kuwa:

i. Taarifa na mihutasari kama vile Kadi ya Muhtasari wa Taarifa ya Shule, mabango, vipeperushi, zinarahisishwa.
ii. Taarifa zinawasilishwa kwa haraka kwa taasisi husika/watumiaji (wamiliki wa shule, Idara ya Uthibiti Ubora) kwa hatua.
iii. Taarifa zilizorahisishwa na mihtasari zinasambazwa kwa kiasi kikubwa kwa wadau, ikiwa ni pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa na wanajumuia wa shule.
iv. Taarifa zinazoonyesha maeneo yanya mafanikio na udhaifu/mapengo ili kuweza kuyatambua na kuchukua hatua za kuzishughulikia mapengo yaliyoripotiwa.
v. Tamaduni nzuri kutoka kwenye shule zinazofanya vizuri yanakuzwa kwenye shule zinazofanya vibaya katika masomo.
vi. Taarifa na mapendekezo yake yanatekelezeka na kila mhusika wa Uthibiti Ubora.

### 3.2.1 Ufuatiliaji

Idara Idara ya Uthibiti Ubora wa Shule italazimika kufanya ukaguzi wa ufuatiliaji wa Shule/Vyuo Vya Ualimu/Programu za Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi zilizokwisha kaguliwa ili kupima ni kwa kiasi gani ushauri na mapendekezo yaliyotolewa yamefanyiwa kazi. Hivyo basi;

- Ukaguzi wa ufuatiliaji wa lazima utalazimika kufanyika kwa shule zote zilizofanya vibaya ndani ya siku 60 baada ya Ukaguzi wa mwisho wa Ujumla wa Shule kufanywa na Maafisa Uthibiti Ubora wa Shule kutoka nje, ili kuthibitisha kama mapendekezo yaliyotolewa yamezingatiwa.
- Kulingana na majibu yaliyopendekezwa, kaguzi za ufuatiliaji za kupima utekelezaji wa mapendekezo ya muda mfupi yaliyotolewa kuhusu shule zitafanywa katika ngazi ya shule/jamii kila robo mwaka, wakati utekelezaji wa mapendekezo ya muda mrefu yatafuatiliwa kila baada ya miezi sita.
- Wathibiti Ubora wa Shule watawasilisha masuala yanayohitaji kutekelezwa kwa Walimu Wakuu/Wakuu wa Shule/Vyuo, na Maafisa Elimu Kata, kwa kutumia Jedwali rahisi wakionesha changamoto zilizoibuliwa, mapendekezo ya muda mfupi na mrefu, muda wa utekelezaji na mtekelezaji husika.
- Kwa ajili ya uwajibikaji, kila ngazi ya utekelezaji wa Uthibiti Ubora wa Shule itatakiwa kuwa na jalada la kumbukumbu au fomu ya kujitathmini ili kufuatilia utimizaji wa malengo au ikionesha kama chombo/ofisi husika imekidhi viwango na kanunu au la.

04

SEHEMU YA


# NNE

# MFUMO WA UENDESHAJI WA UTHIBITI UBORA WA SHULE

## MFUMO WA UENDESHAJI WA UTHIBITI UBORA WA SHULE

Ni muhimu kuhakikisha kuwa Mfumo wa Uthibiti Ubora wa Shule unafanya kazi kwa ufanisi zaidi ili kufikia matokeo bora ya kujifunza na kwamba wanazingatia Sera, Sheria, Kanuni, na vigezo vingine e vya viwango vya ubora vilivyowekwa kusimamia utoaji wa elimu. **Kielelezo Na 3** kinaonesha namna ya utekelezaji wa mfumo wa Uthibiti Ubora wa Shule.

Kielelezo Na. 3. Utekelezaji wa Mfumo wa Uthibiti Ubora wa Shule





### 4.1 Utendaji kazi wa Uendeshaji

Usimamizi wa ufanisi wa utendaji wa Mfumo wa Uthibiti Ubora wa Shule utaeleza kwa uwazi wahusika muhimu na sifa za jumla zinazohitajika ili utendaji wao uwe

bora. Zifuatazo ni sifa zinazohitajika za wahusika katika viwango tofauti, **Kielelezo Na. 4** kinabainisha sifa hizo

Kielelezo Na. 4 Mfumo wa Uendeshaji wa Uthibiti Ubora wa Shule




### 4.1.1 Ngazi ya Taifa

Katika ngazi ya kitaifa, Idara ya Uthibiti Ubora wa Shule itaongozwa na Mkurugenzi wa Uthibiti Ubora wa Shule, akisaidiana na Wakurugenzi Wasaidizi wa Awali, Msingi, Sekondari, Vyuo vya Mafunzo ya Elimu ya Msingi, Maafisa Uthibiti Ubora wa Shule wa Masomo na wafanyakazi wa kiufundi. Wakurugenzi wasaidizi wa elimu ya msingi, sekondari, na ualimu pia watatoa huduma kwa shule za awali, msingi, sekondari, vyuo vya walimu, na elimu maalum, watu wazima, na elimu isiyo rasmi. Aidha, kutakuwa na wasimamizi wa masomo na wafanyakazi wa kiufundi katika ngazi ya kitaifa. Zaidi ya hayo, Idara ya Uthibiti Ubora wa Shule itakuwa na jukumu la kuhakiki ubora katika michakato ya utawala, usimamizi, na utoaji wa elimu katika ngazi zote za Uthibiti Ubora wa Shule, ikiwa ni pamoja na ngazi za kikanda, wilaya, na kata na kutoa mapendekezo ya kuboresha.

Wahusika katika ngazi hii watakuwa na jukumu la kusimamia na kuratibu shughuli za Uthibiti Ubora wa Shule katika ngazi ya kitaifa na kuanzisha na kudumisha uhusiano na watendaji wengine ndani ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) wenye majukumu ya kuweka viwango kama ilivyoelezwa katika maelezo yao ya kazi. Wafanyakazi wa kiufundi katika kila ngazi ya Uthibiti Ubora wa Shule watakuwa na jukumu la kutoa msaada wa kiufundi katika kurahisisha taratibu za utawala na uendeshaji, ikiwa ni pamoja na usafiri, mawasiliano, na ununuzi wa vifaa na kazi za kawaida za ofisi. Wafanyakazi wa kiufundi pia watahakikisha kuwa Kadi ya Muhtasari wa Taarifa ya Shulezinafanyiwa marekebisho na kuonyeshwa kwenye ubao wa taarifa za shule. Kadi ya Muhtasari wa Taarifa ya Shule pia zitapakiwa kwenye Mfumo wa Kidigitali wa Uthibiti Ubora wa Shule.

### 4.1.2 Ngazi ya Mkoa

Ofisi ya mkoa itaongozwa na Ofisa Mkuu Mthibiti Ubora wa Shule wa Mkoa, ambaye atawajibika kwa Mkurugenzi wa Idara ya Uthibiti Ubora. Katika ngazi hii, shughuli zifuatazo zitafanyika:

i. Kufanya shughuli za uthibiti ubora kama mthibiti ubora wa nje katika eneo la mkoa wake.
ii. Kufanya uchunguzi wa mara kwa mara wa hali ya halisi ya shule, vyuo, na vituo na kupendekeza hatua za marekebisho.
iii. Kufuatilia na kutathmini ubora na utekelezaji wa mipango ya uthibiti ubora na huduma wa ndani katika eneo la mkoa.
iv. Kuandaa, kuchambua, na kupakia taarifa kwenye Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Sekta ya Elimu kulingana na mfumo wa kazi na itifaki iliyokubaliwa.
v. Kusimamia na kusaidia shughuli za uthibiti ubora wa shule katika eneo la kikanda.
vi. Uratibu na kutoaji ushauri katika masuala yanayohusu uthibiti ubora wa shule katika ngazi za awali, msingi, elimu ya watu wazima, na elimu maalum (ualimu na vyuo vya maendeleo ya wananchi) na shule zisizo rasmi katika mkoa.
vii. Kuandaa ripoti za tathmini za shule za awali, sekondari, zisizo rasmi, ualimu, na vyuo vya mafunzo na kusambaza matokeo yao kwa wadau.
viii. Kusimamia masuala ya fedha, akaunti na shughuli za ununuzi na usambazaji.
ix. Kusimamia masuala ya mawasiliano na itifaki.
x. Kusimamia majukumu ya utawala na rasilimali watu.
xi. Kutoa ushauri kwa mkurugenzi kuhusu masuala yanayohusiana na uthibiti ubora katika ngazi ya mkoa.
xii. Kuandaa na kuwasilisha ripoti mara kwa mara kama inavyohitajika na utaratibu wa wa idara au kama ilivyoelekezwa.

### 4.1.3 Ngazi ya Wilaya

i. Kusimamia shughuli za uthibiti ubora wa shule katika utoaji wa elimu ya awali, msingi, sekondari, ikiwa ni pamoja na ualimu, vituo vya elimu, mahitaji maalum, elimu ya watu wazima na elimu isiyo rasmi katika ngazi ya wilaya, na kuandaa ripoti za mara kwa mara.
    a) Kutembelea shule nzima kwa minajili ya kutathmini na kuona maendeleo yaliyofikiwa.
    b) Kufanya ziara za ufuatiliaji wa tathmini ya utekelezaji.
    c) Kufanya ziara maalum.
    d) Kutoa ushauri juu ya masuala yanayohusiana na uthibiti ubora katika shule za awali, msingi, elimu ya watu wazima na elimu maalum.
    e) Kuwajengea uwezo walimu utakaopelekea ufanisi wa uthibiti ubora wa shule katika taasisi zao.
    f) Kuandaa ripoti za tathmini na kuwasilisha matokeo yake kwa wadau.
    g) Kukusanya takwimu mbalimbali za elimu, kuchambua na kuandaa taarifa na kuziwasilisha kwa mamlaka husika
    h) Kufanya utafiti wa msingi wenye kunuia kutatua changamoto juu ya utoaji wa elimu ya awali, msingi, watu wazima, na elimu maalum na kushauri ipasavyo.

ii. Kusimamia masuala ya fedha, akaunti na shughuli za ununuzi na usambazaji.
iii. Kusimamia masuala ya mawasiliano na protokali katika masuala ya kiofisi
iv. Kusimamia masuala ya kiutawala na rasilimali.

### 4.1.4 Ngazi ya Kata

Mtendaji mkuu katika ngazi ya kata atakuwa Afisa Elimu wa Kata, ambaye atapewa jukumu la kufanya ukaguzi wa shule katika shule zilizo ndani ya kata kulingana na maelekezo ya kazi yake. Hii itajumuisha, pamoja na mambo mengine, kuanzisha na kudumisha uhusiano na Mamlaka za Serikali za Mitaa, kutoa mafunzo na ushauri kwa walimu na wakuu wa shule, na kukuza kampeni za kuhamasisha jamii kuhusu masuala yanayohusu shughuli za Uthibiti Ubora wa Elimu katika shule kwa ngazi ya kata.

### 4.1.5 Ngazi ya Kijiji/Mtaa

Mtendaji mkuu katika ngazi ya kijiji/mtaa atakuwa Afisa Mtendaji wa Kijiji/Mtaa. Majukumu yake muhimu yatakuwa ni kushirikiana na Kamati ya Maendeleo ya Kata, Afisa Elimu Kata, na Timu ya Usimamizi wa Shule, kuhamasisha ushirikishwaji wa jamii katika shughuli za Uthibiti Ubora wa Elimu katika ngazi ya kijiji, na kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa na Maafisa Uthibiti Ubora kutoka nje.

### 4.1.6 Ngazi ya Shule

Watendaji wakuu katika ngazi ya shule watajumuisha wakuu wa shule, wakuu wa vyuo, walimu, wakufunzi, Timu ya Usimamizi wa Shule, Timu ya Usimamizi wa Chuo, Kamati/Bodi ya Shule, Chama cha Wazazi na Walimu na Wathibiti Ubora wa Elimu wa Ndani. Wajibu wa kila mtendaji ni kama ifuatavyo:

- Wakuu wa shule/ vyuo, kwa kushirikiana na Kamati za Utendaji za Shule au Kamati za Utendaji za Chuo, watahakikisha kuwa mtaala, sera na maelekezo yanatekelezwa kwa ukamilifu.
- Walimu/wakufunzi watahusika na kufundisha darasani, kutathmini na kufuatilia maendeleo ya kitaaluma kwa njia ya kutafakari kila mara na kuchukua hatua dhidi ya vitu wanavyofanya darasani.
- Kamati/bodi ya shule/chuo, kwa niaba ya jamii, watashirikiana na wakuu wa shule/vyuo, walimu/wakufunzi kuandaa Mpango wa Jumla wa Maendeleo ya Shule na kusimamia shughuli za kila siku za shule kwa ushirikiano na Timu ya Usimamizi wa Shule/Chuo.
- Timu ya Wathibiti wa Elimu wa Ndani itafuatilia na kutathmini mchakato wa utekelezaji wa mitaala na tathmini ili kuwajulisha mara kwa mara watendaji husika kuhusu mbinu mbadala za ubora.

## 4.2 Sifa za Jumla za Watendaji Wakuu

Pamoja na mambo mengine, watendaji wakuu watakuwa na sifazifuatazo:

### a) Sifa za Chini za Kuingia

- Maafisa Uthibiti Ubora wa Shule watakuwa na shahada ya kwanza katika elimu, au zaidi na uzoefu wa kufundisha darasani wa angalau miaka kumi.

- Afisa Elimu Kata atatakiwa kuwa na shahada ya kwanza au zaidi, na awe mwalimu mwenye sifa na uzoefu wa angalau miaka saba, vilevile adhihirishe umahiri katika usimamizi.

### b) Mchakato wa Ajira

Ofisa Mkuu Mthibiti Ubora wa Shule wa Mkoa na Ofisa Mkuu Mthibiti Ubora wa Shule wa Wilaya atabainisha walimu wenye uwezo katika ngazi husika (awali na kuendelea) na kuwapendekeza kwa ajili ya mahojiano na kisha uteuzi wa kuwa katika Timu ya Wathibiti Ubora wa Shule. Katika kuajiri maafisa elimu wa kata, kama msimamizi wa karibu na shule, mamlaka husika itajikita katika umahiri zifuatazo:

- Umahiri wa kufundisha.
- Ufuatishaji wa maadili na kanuni ya maadili walimu.
- Uzoefu katika vyeo vya uongozi, mfano, mwalimu mkuu, makamu wa mwalimu mkuu, au mwalimu wa taaluma.
- Uzoefu wa angalau miaka saba katika ualimu.
- Kuonesha uwezo wa usimamizi kama vile ujuzi wa mawasiliano na ujuzi wa kibinafsi, kuandika taarifa, kupanga, n.k.

### c) Mafunzo ya Awali

Maafisa Uthibiti Ubora wa Shule wapya watapewa kozi ya mafunzo ya awali ya miezi minne (ikiwa ni pamoja na wiki mbili za kushiriki katika shughuli za uwandani na kipindi cha majaribio cha mwezi mmoja), ambapo Afisa Mthibiti Ubora wa Shule mwenye uzoefu atawafunda kabla ya kuthibitishwa kuwa Maafisa Uthibiti Ubora wa Shule kamili na Waziri wa Elimu. Mada za mafunzo yataainishwa na Mwongozo wa Mafunzo ya Maafisa Uthibiti Ubora wa Shule.

Maafisa Uthibiti Ubora wa Shule watawasaidia wakuu wa shule/vyuo, na walimu wakati wa ziara za Ukaguzi wa Elimu. Vilevile, watawasadia maafisa elimu kata katika kusimamia na kufunda wakuu wa shule/vyuo. Hii itakuwa ni kazi ya kila siku za Maafisa Uthibiti Ubora.

### d) Ujenzi wa Uwezo Endelevu

Hii itategemea mahitaji ya kitaalamu ya Maafisa Uthibiti Ubora wa Shule kuendana na mageuzi ya utoaji wa elimu au haja inayoongezeka ya kuboresha ujuzi wa utendaji katika shughuli maalum za Uthibiti Ubora wa Elimu.

## 4.3 Maadili ya Mthibiti Ubora wa Shule wa Ndani

### 4.3.1 Uthibiti Ubora wa Shule wa Ndani

Mkuu wa shule, kama Mthibiti Ubora wa Ndani ya Shule, anatarajiwa kuzingatia kanuni za maadili zilizotolewa na mwajiri. Aidha, wathibiti ubora wa Ndani ya Shule lazima wafuate kanuni za kitaalamu ya maadili kama iliyoelezwa katika kitabu cha mwongozo wa wakuu wa shule.

### 4.3.2 Maafisa Uthibiti Ubora wa Karibu na Shule

Maafisa Elimu wa Kata wana jukumu la kusimamia shule kwa njia ya usimamizi wa karibu na shule. Wanatarajiwa kuzingatia kanuni za maadili zilizotolewa na mwajiri.

### 4.3.3. Maafisa Uthibiti Ubora wa Shule wa Nje

Afisa Mthibiti Ubora wa Shule wa mfano ni yule anayetambua kuwa kazi ya mwalimu darasani na malezi ya watoto kwa ujumla si rahisi, na kwamba anafanya kazi hiyo kiuweledi wa kazi bila upendeleo, ubaguzi, na kuheshimu sheria na kanuni husika na kuwa na mtazamo chanya. Hivyo basi, Afisa Mthibiti Ubora wa Shule (AMUS) ni lazima azingatie kanuni za kimaadili za kazi yake kama zilivyofafanuliwa katika Kiongozi cha Mthibiti Ubora wa Shule (KMUS).

### 4.3.4 Utawala

Mfumo wa Uthibiti Ubora wa Shule itasimamiwa na ofisi mbalimbali za kitaifa, kimkoa, kiwilaya, kikata, kikijiji/kimtaa, na kishule. Katika ngazi ya taifa, kutakuwa na mkurugenzi wa Idara ya Uthibiti Ubora Shuleni, na wasaidizi wa mkurugenzi, mmoja kwa kila sehemu ya msingi, sekondari, usimamizi, na utawala. Kila sehemu itajumuisha timu ya Wathibiti Ubora wa Elimu wa Ndani ambao ni wataalamu wa masomo husika watakaowajibika kwa kuratibu mikoa na masuala yanayohusiana na masomo yao.

Katika ngazi ya mkoa, kutakuwa na Ofisa Mkuu Mthibiti Ubora wa Shule wa Mkoa ambaye atapata msaada kutoka kwa Naibu Ofisa Mkuu Mthibiti Ubora wa Shule wa Mkoa, pamoja na Ofisa Mkuu Mthibiti Ubora wa Shule wa Mkoa kwa masomo ya sekondari na elimu ya walimu, na wakurugenzi wa sehemu ya shule za msingi. Katika ngazi ya Wilaya, kutakuwa na Ofisa Mkuu Mthibiti Ubora wa Shule wa Wilaya ambaye atapata msaada kutoka kwa Naibu Ofisa Mkuu Mthibiti Ubora wa Shule wa Wilaya na timu ya Maafisa Uthibiti Ubora wa shule kwa masomo ya shule za msingi.

Shughuli za Uthibiti Ubora wa Shule katika ngazi ya kata zitafanywa na Afisa Elimu wa Kata, msimamizi wa karibu wa shule, ambaye atahitajika kufanya mikutano ya kila mwezi na wakuu wa shule/vyuo na walimu. Katika ngazi ya kijiji/mtaa, wazazi/jamii watahusishwa katika kuboresha ubora wa shule na utendaji wa wanafunzi na kukuza nidhamu yao. Katika ngazi ya shule, Timu ya Wathibiti wa Elimu wa Ndani itafanya tathmini za shule yenyewe na kuandaa mpango wa kuboresha mkakati. Maafisa Uthibiti Ubora wa Shule watasaidia shule kwa kuelekeza mambo yanapaswa kujumuishwa katika mpango wa kuboresha shule, na afisa elimu kata watasaidia kuhakikisha kuwa mpango unazingatiwa na kwamba maboresho yanafanywa na kurekodiwa.

### 4.3.5 Uratibu

Kupitia Mfumo wa Kidigitali wa Uthibiti Ubora wa Shule, wizara itashirikiana na mashirika, taasisi, na washirika wa maendeleo kutoka ndani na nje ya nchi ambao wanafanya programu za elimu na tathmini kwa lengo la kuboresha elimu nchini. Idara ya Uthibiti Ubora wa Shule itaunda mfumo wa pamoja unaounganisha

vyombo vyote chini ya Wizara ya Elimu na wizara nyingine zinazohusika katika utoaji wa elimu kupitia mfumo wa uthibiti ubora wa elimu uliounganishwa.

### 4.3.6 Muungano

Muungano unahohusisha wizara, taasisi zao, na washirika wa maendeleo katika uthibiti ubora wa shule ni muhimu katika kuhakikisha uratibu, ushirikiano, na msaada wenye ufanisi katika sekta ya elimu. Uhusiano huu husaidia kusawazisha juhudi, na kutumia rasilimali kutekeleza mikakati kamili ya kuboresha elimu. Muungano wenye ufanisi kati ya wizara, taasisi, Mamlaka ya Elimu Tanzania, Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania, Bodi ya Huduma za Maktaba ya Tanzania, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, na washirika wa maendeleo unahitaji njia imara za mawasiliano, malengo yanayoshirikishwa, na dhamira ya kutatua matatizo kwa pamoja. Mazungumzo ya kawaida, mipango ya pamoja, na uelewa wazi wa majukumu na wajibu husika huchangia kwa njia inayoeleweka zaidi na yenye athari katika kuboresha ubora wa shule.

Mahusiano yanaweza kuimarishwa kupitia nyanja tofauti kama vile:

i. Ulinganishaji wa Sera: Wizara za elimu hupanga sera na miongozo ya jumla kwa sekta ya elimu, ikiwemo uthibiti ubora. Mawakala wa ndani ya wizara, kama vile vyombo vya uthibiti ubora, hufanya kazi ya kutafsiri sera hizi kwenda kwenye vitendo:

ii. Mwongozo wa Uthibiti: mara nyingi Wizara na taasisi zilizo chini yake hupanga na kutekeleza mfumo wa uthibiti unaosimamia uendeshaji wa shule na taasisi nyingine za elimu. Washirika wa maendeleo wanaweza kuchangia kwa kutoa msaada wa kiufundi na utaalamu katika kukuza na kutekeleza hatua za uthibiti zenye ufanisi.

iii. Kushirikishana Takwimu na Kwenye Uchambuzi wa Takwimu: Wizara na taasisi hukusanya na kuchambua data kuhusu vipengele mbalimbali vya elimu, ikiwa ni pamoja na viashiria vya ubora. Washirika wa maendeleo wanaweza kusaidia juhudi hizi kwa kutoa zana, utaalam, na ufadhili wa ukusanyaji na uchambuzi wa data.

iv. Ujenzi wa Uwezo: Wizara na taasisi zinazingatia uimarishaji wa uwezo wa wataalamu wa elimu, ikiwa ni pamoja na walimu na waendeshaji wa shule, ili kuboresha elimu. Washirika wa maendeleo wanaweza kutoa programu za mafunzo, rasilimali, na utaalamu ili kusaidia jitihada za kuimarisha uwezo.

v. Uhamasishaji wa Rasilimali: Wizara na taasisi zinafanya kazi ya kuhamasisha rasilimali za kifedha na zisizo za kifedha ili kusaidia jitihada za kuboresha elimu. Washirika wa maendeleo wanaweza kuchangia kwa kutoa ufadhili, msaada wa kiufundi, na rasilimali nyingine kuongeza juhudi za serikali.

vi. Utafiti na Ubunifu: Wizara na taasisi hushiriki katika shughuli za utafiti ili kutambua taratibu bora na njia za ubunifu za kuboresha elimu. Washirika wa maendeleo mara nyingi hutoa msaada kwa miradi ya utafiti na kuchangia maarifa na uzoefu muhimu kutoka katika muktadha mwingine.

vii. Miradi ya Pamoja: Wizara, taasisi, na washirika wa maendeleo wanaweza

kushirikiana katika miradi maalum ya kuboresha ubora wa shule. Miradi hii inaweza kuwa ya maendeleo ya miundombinu, kuimarisha mitaala, mafunzo ya walimu, na kadhalika

viii. Ufuatiliaji na Tathmini: Wizara na mashirika wanawajibu wa kufuatilia na kutathmini ya ufanisi wa hatua za uthibiti ubora wa elimu. Washirika wa maendeleo wanaweza kusaidia juhudi hizi kupitia tathmini huru, tathmini ya athari, na mifumo ya utoaji maoni:

ix. Uenezi na Mawasiliano: Wizara na mashirika wanashiriki katika juhudi za uenezi wa kukuza umuhimu wa ubora wa elimu. Washirika wa maendeleo wanaweza kusaidia katika mikakati ya mawasiliano ili kuongeza uelewa na kupata uungwaji mkono kwa jitihada za uthibiti ubora.

x. Mifumo ya Ushirikiano: Mara nyingi Wizara huanzisha mifumo ya ushirikiano, kama vile kamati za mashirika au vikosi vya kazi, ili kuhakikisha ushirikiano wenye ufanisi. Washirika wa maendeleo hutumia mifumo hii ya ushirikiano ili kuelekeza misaada yao kulingana na vipaumbele vya kitaifa.

xi. Kikundi cha Kufuatilia na Kutathmini Kazi za Kiufundi kitapanuliwa kwa kushirikisha wawakilishi kutoka kila wizara, idara, shirika, na washirika wa maendeleo katika ajenda ya ubora wa elimu.



05

SEHEMU YA

# TANO

# UFUATILIAJI, TATHMINI NA UJIFUNZAJI KATIKA UTHIBITI UBORA WA SHULE

# UFUATILIAJI, TATHMINI NA UJIFUNZAJI **KATIKA UTHIBITI UBORA WA SHULE**

## 5.1 Utangulizi

Ufuatiliaji wa Tathmini na Ujifunzaji ni mchakato wa kina unaosaidia taasisi kuboresha utendaji wao, ufanisi, na mkakati wa taasisi. Ufuatiliaji wa Tathmini na Ujifunzaji ina sehemu kuu tatu, ambazo ni: ufuatiliaji, tathmini, na ujifunzaji. Ufuatiliaji unahusisha kukusanya taarifa na habari kisayansi ili kufuatilia maendeleo, uzalishaji, na matokeo ya mradi au programu. Tathmini hufanyika kwa kina na hutumia mbinu za kisayansi katika kubainisha, umuhimu, ufanisi, athari, na uhakika wa mradi au programu kuendelea kwa muda mrefu. Ujifunzaji unahusisha kutafakari matokeo ya ufuatiliaji na tathmini, utambuzi wa taratibu bora, na utumiaji wa mafunzo yaliyopatikana kuboresha maamuzi ya baadaye, mipango, na utekelezaji. Sehemu hii inajumuisha Ufuatiliaji wa Tathmini na Ujifunzaji katikamchakato wa uthibiti ubora wa shule moja moja na uthibiti ubora wa elimu kwa ujumla wake.

## 5.2 Mwongozo wa Ufuatiliaji wa Tathmini na Ujifunzaji katika Uthibiti Ubora wa Shule

Sehemu hii inatambua umuhimu wa kufuatilia utekelezaji wa Kiunzi cha Uthibiti Ubora wa Elimu ya Msingi, Sekondari, na Ualimu na kutathmini mafanikio ya malengo yaliyowekwa kwa kuchambua mipango iliyotekelezwa kupitia kiunzi hiki. Hii pia inajumuisha kutathmini ufanisi wa kiunzi katika kukusanya na kutathmini data na taarifa muhimu kupitia maeneo nane yaliyowekwa na viashiria vyake. Changamoto, udhaifu, mizozo, mambo yasiyohusika, na taarifa nyingine muhimu zinapaswa kurekodiwa kwa kutumia njia ya kudumu. Mapendekezo ya kufanya marekebisho au kuingilia kati yanaweza kutolewa papo kwa papo au wakati wa ukaguzi. Mapitio ya taarifa ya maendeleo yanatarajiwa kupatikana kwa njia ya kushauriana, ambapo mthibiti wa ndani/nje watapewa jukumu la kutathmini makubaliano kulingana na hadidu rejea. Utekelezaji wa Kiunzi cha Uthibiti Ubora wa Shule kitazingatia ushirikiano kati ya wadau wa elimu na dhamira ya kuboresha utoaji wa elimu bora kwa wanafunzi wote na kwa wakati wote.

Kiunzi kitajumuisha viwango, viashiria, zana za tathmini, maoni, na mipango ya uboreshaji ili kusaidia mamlaka ya elimu, waendeshaji wa shule, na wadau wengine kufuatilia na kuboresha elimu. Wakati huo huo, ili kufikia usimamizi na ufuatiliaji endelevu, watekelezaji wa Kiunzi cha Uthibiti Ubora wa Elimu ya Msingi, Sekondari, na Ualimu katika ngazi zote wanapaswa kuwa na uwezo wa kuelezea na kutathmini maendeleo ya viashiria fulani maalum. Viashiria hivi, miongoni mwa mengine, ni

mwenendo wa idadi ya taasisi zilizotembelewa, ushiriki wa wadau, utendaji wa kitaaluma na matokeo ya wanafunzi katika kuandika kusoma na hisabati.

Ukusanyaji, matumizi, na utoaji taarifa juu ya utendaji ni kipengele muhimu cha kiunzi cha ufuatiliaji na tathmini. Taarifa zinaweza kujumuisha maeneo yenye mafanikio, maeneo yanayohitaji kuboreshwa, na mapendekezo ya kuboresha elimu. Katika muktadha huu, mkazo uwe ni kupigania uwepo wa jukwaa litakalotumika mara kwa mara kutawanya taarifa miongoni mwa wadau kwa haraka na kwa uwazi, matokeo yaliyokwisha fikiwa na yale ya mwisho ya viashiria vilivyowekwa ili kubaini njia kamili na mtazamo mpana kuhusu ubora wa elimu. Pamoja na hayo, Mfumo wa Uthibiti Ubora wa Shule unakaribisha wadau wengine wanaofanya shughuli za tathmini katika elimu kuunga mkono juhudi ili kuzidisha shughuli za Uthibiti Ubora wa Shule kulingana na miongozo. Matokeo ya tathmini inayotokana na ushirikiano huu yatachangia ujenzi na kuboreshaji wa shughuli za Uthibiti Ubora wa Shule na utoaji maoni katika ngazi ya wizara kwa ajili ya kufanya maamuzi. Kwa sasa, baadhi ya zana na programu za tathmini, ikiwa ni pamoja na Baraza la Mitihani Tanzania, Tathmini ya Ujifunzaji kwa Vipindi wa Mahali Popote, Tathmini ya Usomaji kwa Madarasa ya Awali, na Tathmini ya Hisabati ya Madarasa ya Awali, yakiwa yote yanatekelezwa na Research Triangle Institute.

## 5.3 Ufuatiliaji, Tathmini na Ujifunzaji katika Uthibiti Ubora wa Shule

Ufuatiliaji, tathmini, na ujifunzaji ina jukumu muhimu katika kuhakiki ubora wa shule ili kuhakikisha kuwa taasisi za elimu zinatoa wanafunzi wenye uzoefu kupitia mazoezi ya kujifunza kwa vitendo. Taarifa zinazokusanywa katika mchakato wa uhakiki ubora wa shule zinasaidia kwenye maamuzi juu ya sera na ugawaji wa rasilimali. Mchakato wa ufuatiliaji, tathmini, na ujifunzaji unapaswa kutambua maeneo ya kuboresha ndani ya mfumo wa elimu ya msingi, iwe ni kuhusiana na mitaala, njia za kufundishia, miundombinu, au mambo mengine. Wadau wote wanaweza kufanya marekebisho maalum ili kuimarisha ubora kwa kufuatilia na kutathmini ubora wa elimu mara kwa mara. Ufuatiliaji na tathmini hutoa taarifa na ushahidi muhimu ambao waendeshaji wa shule na watengeneza sera wanaweza kutumia kufanya maamuzi yaliyo na msingi. Inasaidia kutambua mikakati yenye mafanikio na maeneo yanayohitaji marekebisho kulingana na taarifa sahihi. Kupitia ufuatiliaji na tathmini, shule na wizara zinaweza kubaini jinsi rasilimali zinavyotumiwa na kuangalia kaama zinaendana na malengo ya shule. Hii inaruhusu ugawaji wa rasilimali kwa ufanisi, na kuhakikisha kuwa fedha, wafanyakazi, na vifaa vinatumika kwa uangalifu katika kusaidia upatikanaji wa elimu bora. Katika kuhakikisha kuwa mafunzo endelevu wanayoyapata Walimu kupitia MEWAKA yanakuwa na matokeo chanya, Wathibiti Ubora wa Shule watafanya ufuatiliaji wa ufundishaji na ujifunzaji darasani. Ufuatiliaji huu utajikita zaidi katika kubaini matumizi ya mbinu mpya ambazo walimu walijifunza wakati wa mafunzo yao. Taarifa za ufuatiliaji zitasaidia katika kutoa msaada endelevu wa Kitaaluma kwa walimu na pia kuibua mahitaji ya mafunzo mapya kwa lengo la kuboresha ujifunzaji nchini.

## 5.4 Sababu za Ufuatiliaji, Tathmini, na Ujifunzaji katika Mfumo Thabiti wa Uthibiti Ubora wa Shule

Ufuatiliaji, tathmini na ujifunzaji ni sehemu muhimu katika uthibiti ubora wa shule unaofanya kazi vizuri. Ufuatiliaji, tathmini na ujifunzaji sharti zijumuishwe katika mchakato, utunzaji wa kumbukumbu na matumizi ya taarifa za uthibiti ubora wa shule kuwezesha shule kuwa na mfumo wa uthibiti ubora wenye mafanikio. Ufuatiliaji na tathmini ni muhimu katika kuanzisha mfumo wa Uthibiti Ubora wa Shule wenye ufanisi katika ngazi ya shule na kutoa taarifa kwa serikali kuhusu maamuzi katika ngazi ya sera ya elimu kwa ujumla. Kwa kutoa taarifa na ushahidi wa kuaminika, ufuatiliaji, tathmini na ufundishaji inachangia katika kufanya maamuzi yanayotokana na ushahidi, kwa ajili ya uboreshaji endelevu, na kuimarisha mfumo wa elimu kwa ujumla wake. Yafuatayo ni sababu za kufanya ufuatiliaji, tathmini na ujifunzaji katika mfumo wa uthibiti ubora wa shule.

i. Inasaidia kuwa na mfumo wa kitaalamu ya kukusanya na kuchambua taarifa zinazohusu elimu na matokeo yake.

ii. Inazalisha ushahidi kuhusu ufanisi wa mikakati mbalimbali ya elimu, hatua za uingiliaji, na sera.

iii. Inasaidia kutathmini ufanisi kwa ujumla wake na ufanisi wa matumizi ya rasilimali za ndani ya shule.

iv. Shule zinaweza kuboresha ugawaji wa rasilimali, ikiwa ni pamoja na fedha, wafanyakazi, na vifaa, ili kusaidia malengo ya elimu na kuboresha ubora kwa ujumla.

v. Ufuatiliaji wa mara kwa mara hubainisha maeneo yanayohitaji kuboreshwa, ili kuleta utamaduni wa kujifunza na kuboresha ndani ya shule.

vi. Inatathmini uunganishaji wa mtaala na viwango vya elimu, malengo ya kujifunza, na mahitaji ya wanafunzi.

vii. Inaweza kutathmini ufanisi wa programu za maendeleo ya kitaalam miongoni mwa walimu.

viii. Inapima na kutathmini matokeo na mafanikio ya wanafunzi.

ix. Inatathmini ufanisi wa jitihada za wazazi na juhudi za kushirikisha jamii katika elimu.

x. Inachunguza ujumuishaji na usawa katika elimu.

xi. Inatoa taariza zinazosaidia utungaji na marekebisho ya sera za elimu katika ngazi ya serikali.

xii. Inatoa taarifa kwa serikali kuhusu ugawaji wa rasilimali kwa taasisi za elimu.


xiii. Inachangia katika kupanga na kukuza mfumo wa elimu.

xiv. Inawezesha ulinganishaji na uchambuzi wa matokeo ya elimu kimkoa au kiwilaya.

xv. Inachangia katika mipango ya muda mrefu kwa nia kutoa uelewa kuhusu mwenendo na mifumo ya matokeo ya elimu. Inaboresha uwajibikaji na uwazi katika mfumo wa elimu.

## 5.5 Mduara wa Ufuatiliaji, Tathmini, na Kujifunza

Ufuatiliaji wa Tathmini na Kujifunza ni muhimu katika kuhakikisha ubora wa shule, kupanga miradi/programu, kutekeleza, na kukamilisha. Shughuli za Ufuatiliaji, Tathmini na Kujifunza zimejumuishwa katika mchakato wa uhakiki ubora wa shule ili kuhakikisha tathmini kamili na uboreshaji endelevu. Mzingo wa Ufuatiliaji wa Tathmini na Kujifunza ni mfumo wa kimkakati wa kusimamia uingizaji wa mazoea ya Ufuatiliaji, Tathmini na Kujifunza katika maisha ya miradi/programu za uthibiti ubora wa shule, kama inavyoonyeshwa katika kielelezo kilichopo hapa chini.




## 5.6 Mduara wa Mradi na Shughuli Zihusianazo na Ufuatiliaji, Tathmini na Ujifunzaji

Mchakato wa uthibiti ubora wa shule huanza na awamu ya tathmini ya mahitaji ya awali, ambapo walimu na wasimamizi wanabainisha mahitaji maalum au masuala ndani ya jamii ya shule yanayohitaji kushughulikiwa. Awamu hii inakusanya uelewa kutoka vyanzo mbalimbali, kama vile taarifa za utendaji wa wanafunzi, maoni ya walimu, uchunguzi wa wazazi, na uchunguzi kwa kushuhudia.

Wazo la kuboresha huanzia katika kujifunza kutoka kwenye miradi iliyofanikiwa katika shule nyingine, miradi ya zamani iliyoimarika, au mashauriano na wadau kama walimu, wanafunzi, wazazi, na wajumbe wa bodi ya shule. Njia hii ya ushirikiano hufanikisha uelewa kamili wa mahitaji na sababu zake.

Mara baada ya mahitaji kubainishwa kwa uwazi, hatua inayofuata ni kuelewa kikamilifu changamoto na athari zake kwa jamii ya shule. Hii inajumuisha kuchunguza matokeo tarajiwa ya kujifunza wanayopata wanafunzi, ufanisi wa walimu, umuhimu wa mtaala, na hali ya shule.
Katika awamu hii, wadau hufikiria suluhisho na hatua za kuingilia kati zilizobuniwa

mahsusi kutatua changamoto zilizobainishwa. Ni muhimu kushirikisha pande zote husika, ikiwa ni pamoja na walimu, waendeshaji, wanafunzi, wazazi, na wanajamii, katika mchakato huu ili kuhakikisha kuwa suluhisho zinazopendekezwa ni halisi na zinazowezekana ndani ya muktadha wa shule.

Baada ya kubainisha changamoto na kubainisha suluhisho zinazowezekana kutatulika, hatua inayofuata ni kubuni mradi kamili wa uthibiti ubora. Mradi huu ni dira ya utekelezaji suluhisho za changamoto za uthibiti ubora wa shule na ushughulikijia wa mahitaji yaliyobainishwa kikamilifu.
Kupanga na kufuatilia, shughuli ya kutathmini, na kujifunza ni sehemu muhimu ya mchakato wa uthibiti ubora wa shule. Hii inafaa kuwajumuishi wadau wakuu wa Ufuatiliaji, Tathmini, na Kujifunza katika kubainisha shughuli muhimu na kuandaa mpango halisi wa kutekeleza shughuli hizo. Shughuli muhimu za Ufuatiliaji, Tathmini, na Kujifunza katika mchakato wa uthibiti ubora wa shule ni pamoja na:

i. Kufanya tathmini ya msingi ili kubaini hali ya sasa ya ubora wa shule na kutambua maeneo ya kuboresha.
ii. kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara wa maendeleo kwa kuangalia viashiria na ufikiaji wa mapema wa malengo.
iii. Kufanya tathmini ya kati ya muhula kutathmini ufanisi wa hatua zilizochukuliwa ili kufanya marekebisho yanayohitajika.
iv. Kufanya tathmini ya mwisho ili kupima matokeo ya jumla ya mradi wa uthibiti ubora na kubainisha mambo yaliyojijitokeza yanayoweza kusaidia juhudi za kuboresha uthibiti ubora katika siku za usoni.

Kwa kuongezea, ni muhimu kuanzisha mifumo endelevu ya kutafakari kuhusu matokeo ya Ufuatiliaji, Tathmini, na Kujifunza na kuyatumia katika kufanya maamuzi na kuboresha utendaji wa mradi. Tafakari kama hizi huimarisha utamaduni wa kujifunza na uboreshaji endelevu ndani ya jamii ya shule.

## 5.7 Mchakato faafu wa Ufuatiliaji, Tathmini na Kujifunza katika Mfumo wa Uthibiti Ubora wa Shule

Ni muhimu kutumia mkakati na mbinu faafu kuhakikisha kwamba Ufuatiliaji, Tathmini, na Kujifunza zinakuwa dira ya uthibiti ubora wa shule wenye kuleta matokeo, endelevu, na faafu. Hapa chini ni kanuni muhimu na mikakati yenye kuboresha ufanisi wa ufuatiliaji na tathmini katika uthibiti ubora wa shule:

i. Kuandaa mwongozo wa Ufuatiliaji, Tathmini Na Ujifunzaji ulio wazi na ambao unaelezea malengo maalum, viashiria vya utendaji muhimu, na malengo yanayohusiana na uthibiti ubora wa shule.
ii. Shirikisha wadau wote husika katika mchakato wa ufuatiliaji, tathmini na ujifunzaji, ikiwa ni pamoja na wanafunzi, wazazi, walimu, waendeshaji, na wanajamii. Kuchochea mbinu ya ushirikishaji katika uthibiti ubora wa shule.
iii. Jenga uwezo wa wafanyakazi wa shule kufanya na kushiriki katika shughuli za ufuatiliaji, tathmini na ujifunzaji kupitia timu ya ndani ya uthibiti ubora wa shule.
iv. Sisitiza umuhimu wa taarifa sahihi, zinazoendana na wakati, na faafu. Hakikisha kuwa njia za ukusanyaji wa taarifa hizi ni za kuaminika na kwamba taarifa zilizokusanywa zinaendana na malengo ya uthibiti ubora wa shule.

v. Tumia teknolojia katika ukusanyaji, uchambuzi, na kutoa taarifa kwa ufanisi. Tumia zana za kidijitali kufanikisha mchakato wa Ufuatiliaji, Tathmini, na Kujifunza ili kuongeza upatikanaji wa taarifa.

vi. Kuendeleza utamaduni wa kuboresha daima matokeo ya Ufuatiliaji, Tathmini, na Kujifunza. Tumia matokeo ya tathmini katika kufanya maamuzi, kufanya marekebisho, na kubadilisha mikakati.

vii. Jumuisha vipengele endelevu katika mfumo wa Ufuatiliaji, Tathmini, na Kujifunza na hakikisha kuwa shughuli za ufuatiliaji zinazingatia athari ya muda mrefu ya mipango ya uthibiti ubora wa shule.

viii. Shirikisha jamii ya eneo husika katika mchakato wa Ufuatiliaji, Tathmini, na Kujifunza ili kuchochea hisia ya umiliki na uwajibikaji wa pamoja katika uthibiti ubora wa shule

ix. Weka mifumo madhubuti ya utoaji wa maoni ili kuhakikisha kuwa matokeo ya tathmini yanawasilishwa kwa wadau wote. Tumia maoni hayo kuchochea maboresho na kushughulikia malalamiko.

x. Chochea ufanyaji wa maamuzi kwa misingi ya utafiti. Hamasisha viongozi wa shule na watunga sera kutumia data za ufuatiliaji, tathmini na ujifunzaji kama msingi wa michakato ya maamuzi.

Ufuatiliaji na Tathmini sharti viwasaidie wathibiti ubora wa shule kufanya usimamizi wa shule na kuathiri sera na utekelezaji wa muhtasari wa masomo kwa kiwango cha juu. Ufuatiliaji na tathmini ya uthibiti ubora wa shule pia inapaswa kuzingatia marekebisho ya miongozo na zana za tathmini kwa njia ya kutathmini ufanisi wao, mipaka, na udhaifu kwa wakati wote wa matumizi yake. Wataalamu wa ndani na nje watafanya mapitio ya zana za uthibiti ubora wa shule ili kuhakikisha kuwa zina weledi faafu.

Ufuatiliaji na tathmini unaweza kufanywa kutokana na taarifa zinazopatikana kwa kuchunguza maeneo nane ya mchakato wa uthibiti ubora wa shule.

Kwa kutumia kanuni na mikakati hii, juhudi za uthibiti ubora wa shule kupitia ufuatiliaji na tathmini zinaweza kuwa na matokeo makubwa, endelevu, na muhimu zaidi. Mbinu hii inahakikisha kuwa mchakato wa tathmini unaingizwa katika mkakati wa kuboresha shule kwa ujumla na unachangia katika maendeleo ya jumla ya taasisi ya elimu.

06

SEHEMU YA

# SITA

## UTEKELEZAJI WA KIUNZI CHA UTHIBITI UBORA WA SHULE

## 6.1 Utangulizi

Sehemu hii inaangazia mbinu za utekelezaji wa kiunzi kilichopitiwa cha Uthibiti Ubora wa Shule (SQAF) katika hatua zinazoweza kutekelezeka. Inatoa mwongozo wa kina kwa Maafisa Uthibiti Ubora wa Shule (SQAOs) na wadau mbalimbali katika ngazi zote za wilaya na mikoa namna bora ya kufanya shughuli za Uthibiti Ubora wa Shule (UUS) kwa ufanisi ili kufikia matokeo bora ya ujifunzaji, ambalo ndilo lengo kuu la Kiunzi cha Uthibiti Ubora wa Shule (SQAF).

Hapo awali, Mwongozo wa Utekelezaji wa SQAF ulikuwepo kama waraka wa peke yake uliotengenezwa kama nyenzo muhimu ya kushughulikia malengo ya uthibiti ubora wa shule kwa kipindi cha miaka minne kuanzia 2017/18 hadi 2021/22, chini ya ufadhili uliotengwa kwa muda huo. Hata hivyo, marekebisho ya SQAF yanalazimu kuundwa kwa mpango endelevu wa utekelezaji wa SQAF ambao unaweza kufanya kazi katika nyakati, mazingira na bajeti tofauti.

Muongozo huu wa Utekelezaji wa SAQF utatumika kama mkusanyiko wa mbinu bora katika shughuli za UUS. Muongozo huu unafafanua mikakati ya kukabiliana na changamoto mbalimbali katika UUS hasa changamoto kukosekana kwa SQAOs wakutosha katika masomo yote, kukosekana na uwiano wa SQAOs na mahitaji ya UUS katika Mikoa na Wilaya husika.

## 6.2 Maeneo Mahususi katika Muongozo wa Utekelezaji Wa Kiunzi cha Uthibiti Ubira wa Shule

Kwa ujumla, lengo kuu la SQAF ni kuimarisha ushiriki, kuhakikisha uwazi, na kupanua ushirikiano wa watendaji wakuu katika UUS, na hivyo kuboresha matokeo ya kujifunza. Ili kufikia lengo hili, muongozo huu umejikita katika maeneo matatu ambayo yanahusisha watendaji mbalimbali wakuu, wakiwemo SQAOs kutoka Makao Makuu (HQ), ngazi ya Mkoa, na Wilaya, Maafisa Elimu wa Wilaya (DEOs), Maafisa Elimu Kata (WEOs), na Timu ya Ndani ya Uhakiki Ubora wa Shule (ISQAT). Ili kuwezesha mfumo wa UUS kufanya kazi kwa ufanisi, ni muhimu kwa wadau wote kutumia muongozo huu kuwaongoza katika utekelezaji wa shughuli za UUS. Katika kufanikisha hilo kuna maeneo matatu muhimu ya kuangazia:

### 6.2.1 Kuweka Malengo ya SQA katika Ngazi za Kitaifa na Kikanda

Eneo hili linasisitiza umuhimu wa kuweka shabaha zilizo wazi, zinazoweza kupimika katika UUS katika ngazi ya kitaifa, kimikoa na kiwilaya. Eneo hili linajumuisha

mikakati ya kuoanisha malengo ya haya na malengo mapana ya elimu na kufuatilia mara kwa mara maendeleo ili kuhakikisha uwajibikaji na uboreshaji endelevu.

Majukumu ya Idara ya uthibiti Ubora wa Shule (SQAD) ni kuhakikishia ubora shule za Awali, Msingi, na Sekondari, Shule Zilizo Katika Mfumo usio Rasmi (Huria), Vyuo vya Maendeleo ya Jamii (FDCs), pamoja na Vyuo vya Ualimu (TCs). Hadi kufikia Mei 2024, Tanzania ilikuwa na jumla ya shule za Msingi 20,642, Shule za Sekondari 6,545 na Vyuo vya Ualimu 80 vinavyofanya kazi vizuri. Hivyo, jumla ya shule zinazohitaji kuhakikishiwa ubora ni 27,267.

Kutokana na idadi kubwa ya Shule na Vyuo zinazohitaji Ziara ya Shule Nzima (WSV) inalazimu kuwa na mbinu ya kimfumo itakayosaidia kuchagua na kuzipa kipaumbele shule kwa ajili ya kutembelewa kulingana na mahitaji na kiwango cha changamoto zinazozikabili shule hizo. Katika miaka ya nyuma, baadhi ya shule zilikuwa zinatembelewa na SQAOs mara nyingi, wakati shule nyingine hazijawahi kutembelewa. Sehemu hii inaweka mkakati wa utekelezaji ili kuhakikisha kuwa shule zote nchini Tanzania zinahakikishiwa ubora chini ya SQAF kiliyofanyiwa marekebisho, na kuhakikisha kuwa shule zinazohitaji msaada mkubwa zaidi zitapewa kipaumbele cha juu katika mikakati ya UUS.

Ni muhimu kutambua kuwa mkakati wowote wa UUS unatakiwa kuandaliwa kwa kutumia takwimu zinazopatikana kutoka vyanzo vya kitaifa kama vile Mfumo wa Ufuatiliaji na Taarifa za Elimu (EMIS) na NECTA, pamoja na kumbukumbu za SQAD yenyewe. Taarifa sahihi kulingana na idadi halisi ya SQAOs na idadi ya Shule na Vyuo zilizopo ili kuweka malengo ya utekelezaji wa UUS kwa kipindi fulani. Taarifa sahihi huwezesha kuweka kipaumbele kwa malengo ya UUS dhidi ya rasilimali zilizopo. Kwa kuwa idadi ya SQAOs zilizopo na idadi ya shule zinazohitaji kutembelewa itatofautiana kulingana na wakati, malengo ya UUS na bajeti vinapaswa kuangaliwa ipasavyo, na kwa hivyo utendakazi wa SQAF utahitaji kupitiwa mara kwa mara.

SQAD inapaswa kuhakikisha kuwa kila shule inahakikishiwa ubora kwa muda fulani (k.m. miaka minne). Mipango inapaswa kuundwa kila mwaka katika ngazi ya Taifa, Mkoa na Wilaya ili kujua idadi ya shule zitakazotembelewa kila mwaka. Katika mipango hii kila shule itatambuliwa na taarifa zake kutumwa Makao Makuu ya SQAD, ambayo itasaidia wadau wote kupanga shughuli za UUS kwa mwaka husika.

Kwa hiyo ni muhimu mipango ifuatiliwe kwa karibu, huku tathmini ikifanyika kila robo mwaka. Hii itahakikisha kwamba idadi inayolengwa inafikiwa. Iwapo hakuna mafanikio yanaonekana, basi mipango hiyo inapaswa kusasishwa ipasavyo ili kuhakikisha kuwa malengo ya Wilaya, Mkoa na Kitaifa bado yanafikiwa.

Majedwali yafuatayo yametolewa kama mifano namba mpango UUS unaweza kunafanywa kwa muda wa miaka minne kuanzia 2024/25 - 2027/28.

## JEDWALI 1: IDADI YA SHULE ZITAKAZO TEMBELEWA SHULE KATI YA 2024/25 - 2027/28

| Mwaka wa Fedha | No. ya Shule za Msingi *(Serikali & Binafsi)* | No. ya Shule za Sekondari *(Serikali & Binafsi)* | No. ya Vyuo vya Ualimu *(Serikali & Binafsi)* | Jumla ya Ziara Zilizofanyika |
|---|---|---|---|---|
| Julai - Juni 2024/25 | 5,161 (25% ya shule zote) | 1,636 (25% ya shule zote) | 20 (25% ya vyuo vyote) | 6,817 |
| Julai - Juni 2025/26 | 5,161 (25% ya shule zote) | 1,636 (25% ya shule zote) | 20 (25% ya vyuo vyote) | 6,817 |
| Julai - Juni 2026/27 | 5,160 (25% ya shule zote) | 1,636 (25% ya shule zote) | 20 (25% ya vyuo vyote) | 6,816 |
| Julai - Juni 2027/28 | 5,160 (25% ya shule zote) | 1,637 (25% ya shule zote) | 20 (25% ya vyuo vyote) | 6,817 |
| **Jumla ya WSV** | **20,642** | **6,545** | **80** | **27,267** |

## JEDWALI 2: IDADI YA SHULE ZITAKAZO FUATILIWA KATI YA 2024/25 – 2027/28

| Mwaka wa Fedha | No. ya Shule za Msingi *(Serikali & Binafsi)* | No. ya Shule za Sekondari *(Serikali & Binafsi)* | No. ya Vyuo vya Ualimu *(Serikali & Binafsi)* | Jumla ya Ufuatiliaji uliofanywa |
|---|---|---|---|---|
| Julai - Juni 2024/25 | 1,290 (20% ya shule zote) | 327 (20% ya zote) | 4 (20% ya Vyuo vyote) | 1,621 |
| Julai - Juni 2025/26 | 1,290 (20% ya shule zote) | 327 (20% ya zote) | 4 (20% ya Vyuo vyote) | 1,621 |
| Julai - Juni 2026/27 | 1,290 (20% ya shule zote) | 327 (20% ya zote) | 4 (20% ya Vyuo vyote) | 1,620 |
| Julai - Juni 2027/28 | 1,290 (20% ya shule zote) | 328 (20% ya zote) | 4 (20% ya Vyuo vyote) | 1,620 |
| **Jumla ya FSVs** | **5,161** *(20% ya shule zote)* | **1,309** *(20% ya shule zote)* | **12** *(20% ya Vyuo vyote)* | **6,482** |

## JEDWALI 3: NAMBA YA SHULE ZITAKAZOTEMBELEWA KATIKA ZIARA MAALUMU 2024/25 – 2027/28

| Mwaka wa Fedha | No. ya Shule za Msingi *(Serikali & Binafsi)* | No. ya Shule za Sekondari *(Serikali & Binafsi)* | No. ya Vyuo vya Ualimu *(Serikali & Binafsi)* | Jumla ya Shule Maalumu zilizotembelewa |
|---|---|---|---|---|
| July - June 2024/25 | 206 (ya shule zote) | 65 (4% ya shule zote) | 0 | 271 |
| July - June 2025/26 | 206 (ya shule zote) | 65 (4% ya shule zote) | 0 | 271 |
| July - June 2026/27 | 207 (ya shule zote) | 66 (4% ya shule zote) | 0 | 273 |
| July - June 2027/28 | 207 (ya shule zote) | 66 (4% ya shule zote) | 0 | 273 |
| **Total Number of SSVs** | **826** *(4% ya shule zote)* | **262** *(ya shule zote)* | **0** | **1,088** |

**NB:** Taarifa katika mifano haijumuishi Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Shule zilizo katika Mfumo usio rasmi

### 6.2.2 Matumizi Bora ya Taarifa za Uthibiti Ubora wa Ndani ya Shule

Hatua hii inatoa mwongozo wa jinsi ya kukusanya, kuchambua na kutumia kwa utaratibu taarifa kutoka shuleni ili kufahamisha michakato ya kufanya maamuzi. Kwa kutumia taarifa za ndani zz timu za uthibiti ubora za ndani ya shule, SQAD inaweza kutambua maeneo ya kuboresha, kufuatilia maendeleo, na kutekeleza mikakati inayotokana na ushahidi ili kuimarisha ubora wa elimu.

Kutumika kwa ufanisi taarifa za timu za uthibiti ubora wa ndani ya katka kuhakikisha ubora wa shule ni hatua muhimu katika kuimarisha mchakato mzima wa USSa, hasa katika kukabiliana na changamoto zinazotokana na ukosefu wa SQAOs wa kutosha wenye utaalamu wa masomo na vikwazo vya kijiografia. Mbinu hii inaweza pia kuisaidia SQAD katika kupanga ziara za shule, kuweka kipaumbele kwa afua, na kugawa rasilimali kwa ufanisi. Mbinu hii Inasisitiza muhimu wa timu za ndani ya shule za uthibiti ubora katika kuimarisha shughuli zote za UUS.

Zinapotumiwa vyema,taarifa za timu za uthibiti ubora wa ndani ya shule unaweza kuwa msingi wa shughuli zote za UUS na kuwasaidia sana SQAOs mikoani na wilayani. Taarifa hizi zinaweza kutoa picha ya kina na sahihi ya ufaulu na ubora wa Elimu wa kila shule, taarifa za uthibiti ubora za ndani ya shule huwezesha kufanya maamuzi kwa ufahamu zaidi na kuhakikisha kwamba juhudi zinaelekezwa pale zinapohitajika zaidi. Mbinu hii sio tu kwamba huongeza ufanisi wa ziara za SQAOs katika shule lakini pia inakuza utamaduni wa shule kujitathmini na kujiboresha.

Mabadiliko ya SQAF yanasisitiza umuhimu wa kuunganisha taarifa za timu za ndani ya shule za uthibiti ubora na timu za nje za SQA katika kila kipengele cha mchakato wa UUS. Ujumuishaji huu husaidia kushinda vizuizi vinavyoletwa na vikwazo vya kijiografia na utaalam kwa kuhakikisha kwamba kila shule, bila kujali mahali ilipo, inapata uangalizi na usaidizi unaohitajika kulingana na maarifa yanayotokana na taarifa za ndani za uthibiti ubora. Kwa kuimarisha jukumu la ISQAT na kutumia kwa utaratibu taarifa wanazotoa, tunaweza kuimarisha ufanisi, na usawa wa mchakato wa uthibiti wa ubora, hatimaye kuleta matokeo bora ya elimu kwa wanafunzi wote.

## DWALI 4: UTARATIBU NA MPANGO WA KINA WA MATUMIZI SAHIHI YA TAARIFA ZA TIMU ZA NDANI ZA UTHIBITI UBORA WA SHULE

| SN | Utaratibu | Mikakati | Matokeo Yanayotarajiwa |
|---|---|---|---|
| 1. | Mfumo imara wa kukusanya taarifa | - **Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa:** Kuwepo kwa Mfumo wa pamoja wa kidigitali ambapo shule zote zinaweza kupakia taarifa za ndani za uthibiti ubora. Mfumo huu unatakiwa kuwa rahisi kwa watumiaji, salama, na kufikiwa na timu za uthibiti ubora za ndani na SQAOs ili kwa Pamoja waweze kukagua na kuthibitisha taarifa.<br><br>- **Miundo ya Taarifa Sanifu:** Hakikisha kwamba shule zote zinatumia muundo mmoja na unaofanana kwa ajili ya ukusanyaji wa taarifa ili kuhakikisha uthabiti na urahisi wa uchanganuzi wa taarifa. | Ukusanyaji wa taarifa thabiti na wa kuaminika katika shule zote<br>. |
| 2. | Mafunzo na Kujenga Uwezo | - **Warsha za Mafunzo:** Kufanyika kwa warsha za mara kwa mara kwa timu za ndani za ubora wa ndani ya shule ili kusisitiza jukumu lao muhimu katika kukusanya, kudhibiti na kupakia taarifa kwa usahihi.<br><br>- **Usaidizi Endelevu:** Kutoa usaidizi endelevu na usaidizi wa utatuzi ili kuhakikisha uadilifu na na utoaji wa taarifa sahihi kwa timu za uthibiti ubora wa shule za ndani. | Kuimarisha usahihi, ubora na uaminifu katika taarifa za ndani ya shule |
| 3. | Uchambuzi wa Takwimu na uandaaji wa Taarifa | - **Zana Zinazojiendesha:** Kutumia zana zenye nguvu katika uchanganuzi wa taarifa ili kuchakata nyingi kwa ufanisi, kuwezesha SQAOs kutambua mienendo, kuangazia maeneo ya wasiwasi, na kutoa ripoti za kina.<br><br>- **Uchambuzi wa Wataalamu:** SQAD wanapaswa kushirikiana na wachanganuzi wabobezi wa taarifa kutafsiri taarifa za ndani, wakilenga katika kutambua ruwaza ambazo zinaweza kuonyesha masuala msingi. | Utambulisho bora wa mienendo na masuala, na kusababisha uingiliaji bora zaidi. |
| 4. | Mawasiliano ya mara kwa mara na mrejesho | - **Mikutano ya Mtandaoni ya kila mwezi:** Kufanya mikutano ya mtandaoni kila mwezi na timu za ndani za UUS ili kujadili matokeo ya taarifa, kushirikishana maarifa, na kuongoza maamuzi muhimu.<br><br>- **Mizunguko ya Maoni:** Kuweka utaratibu wa kutoa maoni ambapo timu za ndani zinaweza kupokea maoni yenye kujenga na mapendekezo ya kuboresha kulingana na uchanganuzi wa taarifa zao. | Mawasiliano yaliyoimarishwa na uboreshaji endelevu kulingana na maoni. |
| 5. | Waratibu Takwimu wa Mikoa | - **Uteuzi wa Waratibu wa Mikoa:** Kuwepo kwa waratibu wa mikoa watakao simamia ukusanyaji na usimamizi wa takwimu ndani ya mikoa yao, wakiwa kama kiungo muhimu kati ya shule zilizo katika mikoa yao na makao makuu ya wizara. Hizi zinaweza kuwa ofisi za SQAD za Mikoa<br><br>- **Mapitio ya Mara kwa Mara ya Mikoa:** Kufanya mapitio ya kila robo mwaka ya ubora wa Elimu Kimikoa ili kutathmini ubora wa taarifa zilizokusanywa na kuhakikisha ulinganifu na viwango vya kitaifa. | Kuboresha usimamizi na upatanishi wa taarifa na viwango vya kitaifa. |

| SN | Utaratibu | Mikakati | Matokeo Yanayotarajiwa |
|---|---|---|---|
| 6. | Ziara za Shule Zinazolengwa | - **Ziara Zinazoendeshwa na Taarifa:** Matumizi ya taarifa za ndani za uthibiti ubora zilizochanganuliwa ili kuweka kipaumbele na kupanga ziara za shule, kwa kuzingatia shule zinazoonyesha changamoto maalumu au mikengeuko kutoka kwa ufaulu unaotarajiwa.<br><br>- **Timu Mbalimbali za Taaluma:** Kuunda timu wanataaluma mbalimbali kwa ajili ya kutembelea shule ili kuhakikisha mchanganyiko wa kitaaluma katika kushughulikia mahitaji mahususi yaliyotambuliwa kupitia uchanganuzi wa taarifa za uthibiti ubora wa ndani ya shule | Ziara za shule zenye ufanisi zaidi na zenye matokeo, kushughulikia masuala muhimu. |
| 7. | Ugawaji wa Rasilimali | - **Vifurushi vya Usaidizi:** Kufanya kazi na wadau wengine kuunda na kusambaza vifurushi vya usaidizi kwa shule kulingana na mahitaji yaliyotambuliwa, ikijumuisha nyenzo za ziada za mafunzo, vitabu, nyenzo za kufundishia, au ukuzaji wa kitaaluma unaolengwa.<br><br>- **Usaidizi wa Mbali:** Kutoa usaidizi wa mbali na miongozo ya usaidizi kwa shule za mbali kijiografia ambazo hazina wataalamu mahususi (kama vile walimu). | Usaidizi wa wakati na unaofaa kwa shule, kuimarisha uwezo wao wa uhakikisho wa ubora. |
| 8. | Uboreshaji endelevu | - Mapitio ya Mara kwa Mara ya Mifumo ya Taarifa Kuendelea kutathmini na kuboresha mifumo ya ukusanyaji na uchambuzi wa taarifa ili kukabiliana na changamoto zinazojitokeza na kuhakikisha umuhimu unaoendelea.<br><br>- **Mafunzo ya Kitaaluma:** uwekezaji katika kuwaendeleza SQAOs katika uchakataji na matumizi sahii wa taarifa. | Uboreshaji endelevu wa mifumo ya taarifa na kuimarisha uwezo wa QAOs. |
| 8. | Continuous Improvement | - **Regular Review of Data Systems:** Continuously evaluate and improve data collection and analysis systems to adapt to emerging challenges and ensure ongoing relevance.<br><br>- Professional Development: Invest in the professional development of SQAOs to enhance their data literacy and analytical skills. | Continuous improvement in data systems and enhanced capabilities of SQAOs. |

### 6.2.3 Kufanya Ziara za Uthibiti Ubora wa Shule

Eneo hili linaonyesha taratibu na mbinu bora za kufanya ziara za uthibiti wa ubora wa shule. Eneo hili linaonyesha utayarishaji, utekelezaji, na shughuli za ufuatiliaji zinazohitajika ili kuhakikisha kuwa ziara hizi zinakuwa fanisi katika kutathmini na kuimarisha ubora wa elimu. Hii ni pamoja na kutoa maoni yenye kujenga, kubainisha mbinu bora, na kushughulikia masuala yoyote yaliyotambuliwa ili kusaidia shule katika juhudi zao za kuboresha ujifunzaji na ufundishaji.

Ziara za uthibiti wa Ubora wa Shule ni shughuli muhimu za kuhakikisha uhakikisho wa bora wa elimu unafanyika. Ziara lazima zifanyike kwa ufanisi ili kufikia matokeo yaliyotarajiwa. Kipengele muhimu katika mafanikio ya ziara hizi ni matumizi bora

ya taarifa kutoka kwa ISQAT. Kwa kutumia taarifa hizo, SQAOs wanaweza kupanga na kufanya ziara za uthibiti kwa ufanisi zaidi, na kuhakikisha kwamba rasilimali zinatengwa na kupelekwa kule zinapohitajika zaidi. Taarifa na maarifa za timu za ndani ni muhimu kwa SQAOs wakati wa kupanga ziara zao za shule. Kwa kutegemea taarifa zinazozalishwa ndani, SQAOs wanaweza kuelekeza juhudi zao kwenye shule na maeneo ambayo yanahitaji msaada zaidi. Mbinu hii (Mkakati) ya kutumia taarifa za ndani kabla ya Ziara za SQAOs inahakikisha kwamba ziara za SQAOs zinakuwa bora zaidi na zenye matokeo makubwa na kuhakikisha zinashughulikia masuala muhimu zaidi kwanza. Chini ya mkakati huu, SQAD itafanya aina tatu za ziara shuleni: Ziara ya Shule Nzima (WSV), Ziara ya Kufuatilia Shule (FSV), na Ziara Maalumu za Shule (SSV).

#### 6.2.3.1 Ziara ya Shule Nzima (WSV)

WSV ndiyo aina ya msingi ya tathmini ambayo shule zote zitahitajika kushiriki. Shule zote zitahitajika kuwa na WSV kwa muda wa miaka minne.

#### 6.2.3.2 Ziara ya Kufuatilia Shule (FSV)

Shule iliyotathminiwa kama Dhaifu au Isiyoridhisha katika WSV itatakiwa kufanyiwa FSV. Madhumuni ya ziara hizi ni kubaini kama shule imeweza kufanya mabadiliko katika maeneo ya uboreshaji yaliyoangaziwa katika ripoti ya WSV. FSV itafanyika ndani ya siku 60 baada ya WSV.

#### 6.2.3.3 Ziara Maalumu za Shule (SSV)

SSV hufanyika kwa sababu: -

i. Kama kuna wasiwasi mkubwa, katika usalama wa mwanafunzi na/au changamoto za kimaadili zisiyokubalika, SSV inaweza kutokea bila taarifa ya awali kwa shule na itatekelezwa kwa uharaka mara tu changamoto hizo zitakapotolewa rasmi na Timu ya SQAOs au kuripotiwa kutoka katika chanzo kingine chochote kama suala linalohitaji uangalizi wa haraka
ii. Pia SSV inaweza kufanyika kwenye shule mpya inaomba kibali cha kusajiliwa.

## 6.3 Usambazaji wa SQAO's

SQAD lazima ihakikishe kuwa Mikoa na Wilaya zote zina SQAOs wa kutosha kufanya idadi inayotakiwa ya ziara. Ili kuhakikisha mchakato ufanisi wa wa uthibiti ubora wa shule, kutenga idadi inayofaa ya Maafisa Uthibiti wa Ubora wa Shule (SQAOs) na siku za kutosha kwa kila ziara ya shule ni muhimu.

Jedwali lifuatalo limetengenezwa ili kubainisha idadi ya SQAOs na siku zinazohitajika kufanya ziara ya UUS. Ufanisi katika ziara za UUS unategemea ukubwa wa uwiano wa shule lakini pia inazingatia idadi ya masomo katika taasisi, ikiwa ni pamoja na masomo ya ufundi. Kulingana na mazingira na mahitaji kuna muda katika ziara za uus wataalamu wa masomo ya ufundi wanapaswa kuandamana na SQAOs ili kuleta ufanisi katika ziara UUS. Mbinu hii husaidia kuhakikisha kuwa kila shule inapata uangalizi na usaidizi unaohitajika ili kufikia malengo yake ya uthibiti wa ubora.

## JEDWALI 5: IDADI SQAOS NA SIKU ZA KUTEMBELEA SHULE

| Idadi ya Wanafunzi Shuleni | Namba za siku za kuwa Shuleni | Idadi SQAOs |
|---|---|---|
| 500 na zaidi | 4 | 5 |
| 300 na zaidi | 4 | 5 |
| 300 au chini yake | 3 | 5 |

# MAREJELEO


1. East African Community (2014), *East African Qualifications Framework for Higher Educatio*
2. Idara Kuu ya Utumishi(1998), *Kanuniza Maadili ya Utendaji Katika Utumishi wa Umma Tanzania.*
3. Osaki, K. M (2015), *Standards Setting and Monitoring in Education: The Crucial Role of Education Standards Officers in Quality Assurance; Unpublished paper presented at the Education Week Conference Organized by the Ministry of Education and Vocational Training [MOEVT].*
4. The Inter - University Council for East Africa(2010), *A Road Map to Quality; Handbook for Quality Assurance in Higher Education: Volume 4: Implementation of a Quality Assurance System.*
5. The Inter - University Council for East Africa(2010), *Volume 3: Guidelines for External Assessment at Program Level.*
6. The Inter - University Council for East Africa (2010), *Volume 3: Guidelines for Self-Assessment at Institutional Level.*
7. The Inter - University Council for East Africa(2010), *Volume 3: Guidelines for Self-Assessment at Programme Level.*
8. The Inter - University Council for East Africa (2014), *Principles and Guidelines for Quality Assurance in Higher Education in East Africa.*
9. The Ministry of Education and Vocational Training (1997), *Kiongozi cha MkuuwaShuleyaSekondari Tanzania.*
10. The Ministry of Education and Vocational Training (1997), *School Inspection System (ESDO).*
11. The Ministry of Education and Vocational Training (1999), *Handbook for School Inspectors.*
12. The Ministry of Education Science and Technology Kenya (2000), *Handbook for Inspection of Educational Institutional.*
13. The Ministry of Education, Science, and Technology (2011), *School Supervisor's Training Manual.*
14. The Ministry of Education, Science and Technology (2014), *Education and Training Policy.*

15. The Commission for Universities (2011), *Tanzania Qualification Framework.*

16. The United Republic of Tanzania (2015), *The Functions and Organization Structure of the Ministry of Education, Science and Technology; President's Office Public Service Management, Dar es Salaam.*

17. The Inter-University Council for East Africa (2010): A *Road map to Quality; Handbook for Quality Assurance in Higher Education, Vol. 1*

18. UNESCO (1998), *Supervision and Support Services in Asia volume I-II.*

19. UNESCO (2001), *School Supervision in Four African Countries volume I-II.*

20. *United Republic of Tanzania. The Tanzania Development vision 2025.*

21. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (1991), *Mwongozo wa Shule za Awali.*

22. Ministry of Education, Science and Technology. (2023). *Curriculum for Primary Education, Standard I–VI. Tanzania Institute of Education.*

23. Ministry of Education, Science and Technology. (2023). *Curriculum for Secondary Education, Form I–IV. Tanzania Institute of Education.*

24. Ministry of Education, Science and Technology. (2023). *Curriculum for Secondary Education, Form V–VI. Tanzania Institute of Education.*

25. URT (2023). *New National Education and Training Policy (2023 edition).*